epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Mei 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-



UKURASA 22
**TEN HAG AMJIA JUU MOURINHO**

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581669
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Aliyekuwa Meya Ubungo kortini madai kusambaza taarifa za uongo



• **Pia** yumo Ofisa Jamii Moshi... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 4
### MPANGO WA SAMIA KUPUNGUZA VIFO WATOTO WACHANGA
SERIKALI inakusudia kuanzisha wodi maalum za watoto wachanga (NCU) katika hospitali za halmashauri ili...



UKURASA WA 4
### MBUNGE GEKUL ANG'ANG'ANIWA, AKATIWA RUFANI
MBUNGE wa Babati Mjini (CCM) na Naibu Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria...



UKURASA WA 4
### WANAFUNZI ZANZIBAR WABUNI MFUMO WA ULIPAJI UMEME
WANAFUNZI kutoka shule za msingi nne visiwani Zanzibar wamebuni mfumo unaowezesha malipo ya...



## Mafuriko yaua watu 228 Kenya
UKURASA 19



Baadhi ya marubani na wahudumu wa ndege wakiingia bungeni jijini Dodoma jana kusikiliza Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliyowasilishwa na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



## Ufanisi Bandari wapaa 42%
UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, FLORENT IBENGE KIMEELEWEKA** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Aliyekuwa Meya Ubungo kortini madai kusambaza taarifa za uongo

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Ubungo Dar es Salaam, Boniface Jacob na Ofisa Afya Jamii mkazi wa Moshi, Kilimanjaro, Godlisten Malisa wamepandishwa kizimbani wakikabiliwa na mashtaka matatu likiwamo la kusambaza taarifa za uongo kwa lengo la kupotosha umma kuhusu maiti kukaa siku 12 Hospitali ya Polisi Kilwa Road bila polisi kujua.

Jacob na Malisa walifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na kusomewa mashtaka yao na Wakili wa Serikali, Neema Moshi akisaidiana na Happy Mwakanyamale.

Moshi alidai kuwa Aprili 22, mwaka huu jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Jacob kwa lengo la kupotosha umma, alisambaza taarifa ya uongo kupitia mfumo wa kompyuta wenye jina la Boniface Jacob @ExmayorUbungo wenye kichwa kilichosomeka 'wenye leseni ya kuua wameua tena'.

Wakili huyo alifanunua kuwa taarifa hiyo ya Jacob ilieleza; 'kijana wetu Rajabu Mlanga Mushi maarufu kama Babu G, amekutwa Hospitali ya Kilwa Road akiwa ameuawa. 'Imagine' (fikiri) tumetoa taarifa Jeshi la Polisi la kupotelewa kwa kijana wetu, cha ajabu Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likawa linatusaidia kumtafuta pia'.

"Kila siku Jeshi la Polisi linasema halijapata taarifa wala fununu zozote za kijana wetu na kwamba tuwe wavumilivu wanapambana kuendelea kumtafuta. Jana machale yakawacheza ndugu wa kijana baada ya msiri mmoja kuwatonya ndugu; 'nendeni hospitali ya polisi Kilwa Road mkachungulie vyumba vya kuhifadhia maiti'.

'Ndugu walivyokwenda huko Hospitali ya Polisi Kilwa Road wakamkuta kijana wao akiwa ameuawa, wahusika wa hospitali wanadai maiti ililetwa tangu tarehe 10 Aprili mwaka 2024, na askari wa Jeshi la Polisi'.

'Maiti ina siku 12 katika Hospitali ya Polisi Kilwa Road bila Jeshi la Polisi kujua ipo hapo?...Polisi aliyepeleka maiti ni wa nchi gani? Walipoombwa kujua ni askari wa kituo gani na majina yao ni yapi, wahusika wa hospitali hiyo ya polisi wanadai hawajui na wanaomba wasitajwe...'

'Wacha wanyonge tukazike maiti zetu, sitamani hata kuona ndugu wakiomba uchunguzi dhidi ya maiti yao kwasababu hata mtoto mdogo anajua hapo muuaji ni nani',

'Pili tunajua ile mbinu ya 'TAPE', ile kufunga mtu miguu, kufunga mikono kisha kupigwa 'tape' ya mdomo na puani hadi kifo baada ya ile mbinu ya kupeleka msituni, porini na kupigwa risasi kujulikana. Dar es Salaam ina mtu mmoja katili sana'.

Katika shtaka la pili, Jacob anadaiwa kwamba Machi 19, 2024 jijini Dar es Salaam, alisambaza taarifa ya uongo kupitia mfumo wa kompyuta wenye jina la X, kwa jina la Boniface Jacob @ExMayorUbungo wenye kichwa kisomekacho 'Mauaji Arusha'.

Inaidaiwa kwamba taarifa hiyo ilisomeka 'Mwananchi mwenzetu na aliyekuwa dereva wa magari ya watalii Omary Msamo ameuawa na skari wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha'.

'Omary Msamo ameuawa baada ya kusimamishwa na kushushiwa kipigo kizito kilichopelekea kutoa uhai wake na polisi wa usalama barabarani baada ya kutuhumiwa kuendesha gari akiwa ametumia kilevi'.

'Kwamba, Jeshi la Polisi linatumia kila jitihada kuzuia vyombo vya habari kuripoti tukio hili kama nia ya kuficha na kuwanusuru askari wake dhidi ya mkono wa sheria'.

Iliendelea kudaiwa



kwamba, shtaka la tatu linamkabili mshtakiwa Malisa pekee ambaye anadaiwa kwamba, Aprili 22, mwaka huu ndani ya Jiji la Dar es Salaam, kwa lengo la kupotosha umma alisambaza taarifa za uongo kupitia mfumo wa kompyuta, kwenye akaunti ya Instagram ya jina la Malisa gj.

Taarifa hiyo ilisomeka kwamba 'Aprili 13 Meya mstaafu wa Manispaa ya Ubungo @exmayor bonifacejacob, alitoa taarifa ya kupotelewa na ndugu yake Bw. Robert Mushi maarufu kama Babu G, ambaye alipotea mapema mwaka Aprili 2024'.

'Inadaiwa alikamatwa na watu waliojitambulisha kuwa polisi maeneo ya Kariakoo na baada ya hapo hakuonekana tena'.

'Leo wakaambiwa nendeni hospitali ya polisi Kilwa Road ndugu yenu amefichwa mochwari pale wakaenda. Lahaula! Wakamkuta Robert akiwa katika jokofu la baridi, hakuwa Robert tena bali mwili wake ukiwa na majeraha ya kipigo'.

'Ni mauaji ya kikatili, maskini Robert hajawahi kuwa na ugomvi na mtu, kwanini atendewe haya?

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka hayo, wote walikana. Upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi umekamilika. Kesi imeahirishwa hadi Juni 6, 2024 kwa ajili ya kusomewa hoja za awali.

Washtakiwa wote waliachiwa kwa dhamana, baada ya kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili kila mmoja waliosaini bondi ya Shilingi milioni mbili.

# Ufanisi TPA wapaa asilimia 42

**Na Vitus Audax,** DODOMA

HATUA za uwekezaji zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika maeneo mbalimbali kwenye sekta ya uchukuzi zimetajwa kuzaa matunda ikiwamo kupanda kwa ufanisi kwa asilimia 42.31 katika utolewaji wa huduma za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Hayo yamebainishwa jana bungeni na Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2024/25.

Prof. Mbarawa alisema mafanikio hayo yametokana na TPA kuendelea kuitangaza bandari kimasoko kwa kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

Alisema katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 TPA ilihudumia tani milioni 20.72 ya shehena ikilinganishwa na tani milioni 14.56 ya shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 42.31.

Kuhusu uhudumiaji wa makasha, TPA ilihudumia 805,167 ikilinganishwa na 688,609 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 16.92.

Usafirishaji mizigo kwenda nchi jirani alisema imeongezeka hadi kufikia tani 8,871,438 kwa mwaka 2023 kutoka tani 8,239,112 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 7.67.

Ongezeko hilo la shehena ya mizigo na makasha limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

**MABORESHO BANDARI**

Serikali inaendelea na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, uchimbaji wa kina umefikia mita 15.5 na upanuzi wa lango la kuingia na kugeuzia meli umefikia upana wa mita 200, kwa sasa Bandari hiyo ina uwezo wa kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305.

Aidha, Februari 26, 2024 serikali ilisaini mkataba wa kuendeleza miundombinu ya kupokelea mafuta (SRT) unaohusisha ujenzi wa matangi 15 ya mafuta pamoja na miundombinu yake yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 420,000.

Vilevile, uboreshaji wa Bandari ya Tanga katika awamu ya pili umekamilika kwa asilimia 100 na kuongeza uwezo wa kuhudumia makasha 1,020 TEUs.

Aidha, alisema serikali imeendelea kuboresha bandari zilizopo katika Ziwa Victoria, uboreshaji wa Bandari ya Bukoba umefikia asilimia 47 na Bandari ya Kemondo umefikia asilimia 52.

Kwa mujibu wa Profesa Mbarawa uboreshaji wa Bandari ya Mwanza North umefikia asilimia 40 na kwa upande wa uboreshaji wa Bandari ya Mwanza South unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa baadhi ya miundombinu ya Bandari ya Mwanza North, ili kutoathiri shughuli za kibandari katika mkoa huo.

**VIPAUMBELE 2024/25**

Prof. Mbarawa alisema katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25, wizara hiyo itatumia zaidi ya Sh. trilioni 2.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema wizara hiyo imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo mbalimbali ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea ambayo ni pamoja na ujenzi wa SGR, ukarabati MGR, kuboresha ATCL, ujenzi na ukarabati meli katika Maziwa Makuu.

**SGR**

Kuhusu kuendeleza ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (SGR), Prof. Mbarawa alisema wanatarajia kutumia Sh. trilioni 1.511 kuendeleza katika maeneo yaliyobaki pamoja na ununuzi wa vitendea kazi (vicha na mabehewa).

**MGR KUFUFULIWA**

Aidha, alisema katika kipindi cha mwaka 2024/25 wanatarajia kutumia Sh.bilioni moja kufufua reli iliyopo ya Meter Gauge Railway (MGR) yenye urefu wa kilomita 2,706 katika kipande cha Kilosa – Kidatu chenye Km 108. Pia zitatumia Sh.bilioni 312.03 kufanya ukarabati wa reli iliyopo katika MGR.

**ATCL**

Prof. Makame Mbarawa alisema katika kuendelea kuboresha na kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) Sh.bilioni 324.5 zimetengwa kwa ajili ya kununuliwa ndege tatu, vipuri, injini na kukarabati miundombinu wezeshi.

**MABORESHO MAZIWA MAKUU**

Aidha, alisema Sh. bilioni 190 zitatumika ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu, ambazo ni pamoja na ujenzi wa meli Ziwa Tanganyika ambako utafanyika ujenzi wa meli mpya ya abiria 600 na mizigo tani 400 itakayogharimu Sh. bilioni 25.

Vilevile, alisema serikali itafanya ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 itakayogharimu Sh. bilioni 35, kujenga kiwanda cha kujengea meli chenye uwezo wa kubeba meli zenye uzito wa tani 5,000 kitakachogharimu Sh.bilioni 30 ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 itakayo gharimu Sh.bilioni 20.

**TAA**

Kuhusu ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini (TAA), Prof. Mbarawa alisema zimetengwa Sh.bilioni 108 zinazotarajiwa kutumika katika ujenzi wa kiwanja cha Arusha Sh. bilioni 5.08, ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi, Sh. bilioni 13.

**TAZARA**

Prof. Mbarawa alisema serikali itatumia Sh. bilioni 13 kukarabati na kuboresha Reli ya TAZARA, kuendelea na ununuzi wa rada na vifaa vya hali ya hewa na zitatumika Sh. bilioni 15.

**MABORESHO BANDARI**

Prof. Mbarawa alisema serikali itaendelea kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na bandari nyingine zikiwamo zilizopo katika Maziwa Makuu kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ya TPA.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA: UPUNGUZAJI WA KIWANGO CHA HEWA YA UKAA (KABONI): UHANDISI NA UGAVI WA MIFUMO YA KUHIFADHI UMEME WA BETRI (BESS) KWA AJILI YA MIUNDOMBINU EACOP. - KUMBUKUMBU NA.00000526

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya Ugavi wa Uhandisi, na Ujenzi wa Mifumo ya Kuhifadhi Umeme wa Betri kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Mawanda yanajumuisha uhandisi, ugavi na usafirishaji wa Mifumi Mitano (5) ya Kuhifadhi Umeme wa Betri wa 33 kV, ikiwa ni Pamoja na Kifaa cha kuhifadhia Betri (LFP), Mfumo wa Kubadilisha Umeme (kutoka matumizi ya nishati ya gridi hadi matumizi ya nishati ya nje ya gridi) Vituo vya kufua kusambaza umeme (Transfoma), Mfumo wa ulinzi wa Betri, Mtambo wa Kudhibiti Umeme wenye

- 22MVA/20MWh kwa ajili ya Kituo cha Baharini cha EACOP kilichopo Tanga
- 16MVA/16MWh kwa ajili ya Kituo cha Kusukuma Mafuta namba 6 cha EACOP cha Singida
- 16MVA/16MWh kwa ajili ya Kituo cha Kusukuma Mafuta namba 5 cha EACOP cha Shinyanga
- 16MVA/A/16MWh kwa ajili ya Kituo cha Kusukuma Mafuta namba 4 cha EACOP cha Shinyanga
- 12MVA/12MWh kwa ajili ya Kituo cha Kusukuma Mafuta namba 3 cha EACOP cha Bukoba

Mfumo wa BESS utafungwa na Mkandarasi wa EPC aliyechaguliwa na EACOP. Mgavi wa BESS atatoa usaidizi wa ndani wa Uhakiki wa Ufanisi, Majaribio na Uzinduzi wa Mifumo.

**VIGEZO MUHIMU:**
**kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo**

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu, na uwezo wa kutoa huduma katika wigo husika.
- Maelezo ya miradi au shughuli zinazofanana zilizokwishafanywa zinazotoa uthibitisho wa timu iliyopo yenye weledi , uelewa wa maeneo ya bomba, na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya biashara.
- Cheti cha usajili na Uthibitisho wa usajili wa BRELA wa havi karibuni (ambatanisha nakala)
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Sera YA Haki za Binandamu
- Ubobezi katika Uhandisi na Ugavi wa mifumo ya kutunza wa Umeme wa Betri.
- Pale inapohitajika, uthibitisho wa usajili wa bodi za kitaaluma, kwa mfano Bodi ya usajili ya Wahandisi au Bodi ya Usajili ya Wakandarasi.

---

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **06 Juni 2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000526 – Upunguzaji wa Kiwamgo cha hewa ya Ukaa (Kaboni): Uhandisi na Ugavi wa Mifumo Mitano ya Kuhifadhi Umeme wa Betri kwa ajili ya miundombinu ya EACOP.**

Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.**

---

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya kampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa kampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni ya awali yenye vigezo baada ya kampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA: UPUNGUZAJI WA HEWA YA UKAA: UHANDISI, UNUNUZI, UJENZI NA MAJARIBIO YA UHAKIKI WA UFANISI WA MAUNGANISHO YA GRIDI YA UMEME NA MIFUMO YA BESS YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP). - KUMBUKUMBU NA. 00000527

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Mifumo wa Kuhifadhi Umeme wa Betri na vituo vya kilovolti 33 (33kV) vya Swichi ya Gridi ya umeme kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kusafirisha mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na jumla ya Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Mawanda ya huduma yanajumuisha Uhandisi, Manunuzi, Ujenzi na Majaribio ya Uhakiki wa Ufanisi wa mauganisho ya Gridi ya umeme na mifumoya ya BESS:

- Vituo vya kuunganisha gridi ya kilovoti 33 (33kV) na mifumo inayohusiana na udhibiti na matumizi ikiwa ni pamoja na transfoma za kilovoti 33kV/33kV na vinu vya kusambazia umeme vya kilovoti 33/33kV.
- Mifumo ya BESS ya 33kV pamoja na mifumo yake ya udhibiti (ili kuimalisha umeme wa gridi na kusafirisha umeme uliounganishwa /usio unganishwa kwenye gridi).
- Mifumo ya jumla ya udhibiti wa umeme inayoitwa kwa pamoja Mfumo wa Usimamizi wa Umeme ili kudhibiti na kutoa kipaumbele cha usambazaji wa umeme kwa EACOP.
- Nishati zote zinazohusiana na umeme pamoja na kusimamia uwekaji kebo
- Kazi zote zinazohusiana na ujenzi (barabara za kuingilia, misingi, mitaro, n.k.)
- Mifumo yote inayohusiana na mawasiliano na ulinzi (CCTV, Uzio, Mageti, n.k)

Kwa ajili ya kituo namba 3 cha kusukuma mafuta kilichopo Bukoba, vituo namba 4 na namba 5 vya kusukuma mafuta vilivyopo Shinyanga, kituo namba 6 cha kusukuma mafuta kilichopo Singida na Kituo cha Baharini cha Kuhifadhi Mafuta kilichopo Tanga.

Mifumo ya BESS itatolewa na EACOP bila malipo na itafungwa na kufanyiwa Majaribio ya Uhakiki wa Ufanisi na mkandarasi wa EPC. Kwa hiari yake mwenyewe, Mkandarasi wa EPC ataweza kuwasilisha ofa kwa ajili ya Uhandisi na Ugavi wa mifumo ya BESS ikiwa ni pamoja na Vifaa vya kutunzia Betri, Mifumo ya Usimamizi wa Betri, Vituo vya Transfoma na mifumo ya kubadilisha Umeme.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinzoonesha nia zinatakiwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Maelezo ya shughuli au miradi iliyofanyika inayofanana na huu ambayo ni ushahidi na kuwapo kwa timu enye sifa zinazostahili, uelewa wa maeneo ya bomba la mafuta, na na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya biashara.
- Cheti cha usajili na Uthibitisho wa usajili wa BRELA wa havi karibuni (ambatanisha nakala).
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na fasili ya kampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopo.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na sera ya Haki za Binandamu
- Ubobezi katika Uhandisi, Manunuzi na Ujenzi wa shughuli za Umeme ikiwa ni Pamoja na uzoefu wa kutosha katika Mifumo ya Kuhifadhi Umeme wa Betri.
- Pale Inapofaa, uthibitisho wa usajili wa bodi za kitaaluma, kwa mfano Bodi ya usajili ya Wahandisi au Bodi ya Usajili ya Wakandarasi.

---

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) itumwe kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) au kabla ya tarehe **06 Juni 2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ 00000527 – Upunguzaji wa Hewa ya Kaboni: Uhandisi, ununuzi, Majaribio ya Uhakiki wa Ufanisi wa Maunganisho ya Gridi ya Taifa na Mifumo ya BESS ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika MasharikI (EACOP).**

Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa kuandikwa kwa lugha ya Kingereza.**

---

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakazojumuishwa kwenye orodha ya kampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa kampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni ya awali yenye vigezo baada ya kampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Mpango wa Samia kupunguza vifo watoto wachanga kuanza

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI inakusudia kuanzisha wodi maalum za watoto wachanga (NCU) katika hospitali za halmashauri ili kuboresha huduma na kupunguza vifo vya kundi hilo kutoka vifo 24 kati ya vizazi 1,000 kwa sasa.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika hafla ya uzinduzi wa Mpango Kabambe wa Madaktari Bingwa wa Dk. Samia uliofanyika katika Mkoa wa Iringa.

Katika mpango huo madaktari bingwa watasambazwa katika hospitali za ngazi ya halmashauri na kukaa kwa siku tano wakiwahudumia wagonjwa mbalimbali, ikiwa ni mpango wa Rais Samia wa kuboresha huduma ya afya nchini.

Waziri Ummy alisema kupitia mpango huo wanalenga kusaidia hospitali katika ngazi za halmashauri kuanzisha na kuimarisha wodi maalum za watoto wachanga ili kuokoa maisha ya watoto hao nchini.

Aliwaelekeza madaktari bingwa wa watoto wachanga waliokuwa katika mpango huo kuhakikisha wanaboresha huduma hizo katika hospitali watakazokwenda kuhudumia ili mpaka watakapoziacha ziwe na huduma zilizoimarika.

"Nasisitiza tena kwamba, sambamba na utoaji huduma na kujenga uwezo wa watoa huduma wetu, madaktari bingwa saidieni uanzishaji na kuimarisha utendaji wa NCU kwa kuwa katika mpango huu mtafikia hospitali zote za halmashauri," alisema.

Alisema nchi hiyo bado haijafanya vizuri katika kupunguza vifo vya watoto wachanga kwani takwimu zinaonyesha kuwa vimepungua kwa asilimia nne pekee, kutoka 25 katika kila vizazi hai 1,000 hadi 24 katika vizazi 1,000.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wakiwekeza vizuri katika huduma ya watoto wachanga wanaweza kupunguza vifo hadi asilimia 50.

"Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza pasi na shaka kwamba tukiwekeza kwenye wodi za watoto wachanga tutapunguza vifo vya watoto hao kwa zaidi ya asilimia 50, ndio maana tumeanzisha mpango huu kabambe wa madakatari bingwa ili pia tukaweke msukumo wa kuanzishwa wodi za watoto wachanga," alisema.

Mpango huo pia unakusudia kuboresha huduma nyingine za afya nchini ikiwamo uzazi na wanawake, upasuaji, magonjwa ya ndani, huduma ya ganzi na usingizi hivyo madaktari bingwa katika maeneo hayo watazunguka katika halmashauri zote 184 nchini kutoa huduma.

Aidha, alisema lengo la mpango huo ni kuwajengea uwezo watoa huduma katika maeneo ya kazi, ili kuimarisha utambuzi wa magonjwa, matibabu ya magonjwa, upasuaji na rufani kwa wagonjwa ngazi ya hospitali ya halmashauri.

"Rais Samia ameandika rekodi duniani na barani Afrika ya kupunguza vifo vya wajawazito kwa asilimia 80. Kutoka vifo 556 katika kila vizazi laki moja hadi 104 katika kila vizazi," alisema.

Alisema jumla ya madaktari 95 wapo katika kanda hiyo inayohusisha mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma na watakaa kwa siku tano kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa.

Aidha, serikali inaendelea kuboresha mfumo wa bima ya afya ili kuhakikisha wananchi wote wa kijijini na mijini wanapata huduma bora za afya na katika hilo itasimama kwenye mstari kuhakikisha sheria na kanuni za bima ya afya zinazingatiwa katika uendeshaji wa mfuko huo.

Pia wataanza maandalizi ya Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote ikiwamo kubainisha wasio na uwezo, ili utekelezaji wake utakapoanza kusiwepo malalamiko ya mtu kuachwa.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, alimshukuru Rais Samia kwa kuanzisha mpango huo kwa kuwa utawasaidia wananchi kupata huduma ambayo walilazimika kutumia gharama kubwa na kutembea umbali mrefu ili kuifuata.

"Tunafahamu daktari bingwa gharama yake ya huduma ni kubwa, upatikanaji wake ni mgumu, lakini mmeacha fedha, mmeacha fursa mmeamua kuja kuwahangaikia Watanzania wenzenu hawa," alisema.



Waendesha pikipiki na TOYO wakiwa kwenye foleni eneo la Karume jijini Dar es Salaam jana iliyosababishwa na msongamano wa magari katika barabara ya Uhuru. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbunge Gekul ang'ang'aniwa akatiwa rufani

**Na Godfrey Mushi,** BABATI

MBUNGE wa Babati Mjini (CCM) na Naibu Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, ameendelea kung'anga'niwa baada ya mlalamikaji katika kesi ya udhalilishaji kuweka kusudio la kukata rufani dhidi ya ushindi aliopewa na mahakama.

Mlalamikaji katika kesi hiyo ni aliyekuwa mfanyakazi wake, Hashim Ally, ambaye kupitia wakili wake, Peter Madeleka, amewasilisha rufani namba 5502749 ya mwaka 2024 iliyosajiliwa katika Masijala ya Manyara kwa kutumia mtandao wa Mahakama ya Rufani Tanzania Mei 5, mwaka huu.

Hashim, anapinga uamuzi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, uliotolewa na Jaji Devotha Kamuzora, Aprili 15 mwaka huu, kutupilia mbali kesi dhidi ya mbunge huyo.

Jana, Wakili Madeleka kutoka Kampuni ya Stalwart Law Chambers, anayemtetea Hashim Ally, akizungumza na gazeti hili alisema tayari mteja wake amefungua kesi hiyo.

Aprili 15, mwaka huu katika Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, Mbunge Gekul, alishinda kesi ya rufani ya udhalilishaji iliyofunguliwa na mfanyakazi wake, Hashim, baada ya Jaji Kamuzora, kueleza ilani iliyotumika kumfungulia kesi ya msingi, haikukidhi vigezo.

Katika kesi ya msingi, Gekul alikuwa akikabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababishia madhara ya mwili, chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 iliyofanyiwa Marejeo mwaka 2022.

Alidai kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 1, 2023, Mjini Babati, mkoani Manyara, walimuita Hashim na kumweka kizuizini.

Alidai huku wakimtishia kwa silaha ya moto, walimvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa, jambo lililomsababishia madhara.

# Wanafunzi Zanzibar wabuni mfumo ulipaji umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI kutoka shule za msingi nne visiwani Zanzibar wamebuni mfumo unaowezesha malipo ya umeme kuingia moja kwa moja kwenye mita bila mnunuzi kulazimika kuingiza mita namba za umeme.

Wanafunzi hao walionyesha mfumo huo namna unavyofanyakazi wakati wa maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA yaliyofanyika jijini Arusha.

Shule hizo ni Laureate School of Zanzibar, Bububu Primary School, Turky Primary School na Turkish Marif School za mjini Unguja.

Wakizungumzia mfumo huo walisema utasaidia kurahisisha huduma za umeme kwa watumiaji na kuboresha huduma zinazotolewa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mwanafunzi wa Laureate School Zanzibar, Salina Sharif alisema walibuni mfumo huo kutokana na kuona tatizo la wananchi kushindwa kuunganisha umeme kwa njia ya mtandao.

"Mfumo huu tulioupa jina la Power Pals unatoa suluhisho la mtumiaji wa umeme kuingiza namba za umeme bila kulazimika kuweka namba hizo kwenye mita ya umeme. "Power Pals inakusuluhishia kutia umeme mtandaoni bila ya kwenda nje kujitafutia matatizo," alifafanua.

Mwanafunzi Salina Sharif, alisema ili kutumia mfumo huo mtumiaji atapaswa kuwa ameunganishiwa huduma ya umeme na kifaa cha mita ya kuingiza umeme pamoja na mfumo wa malipo mtandaoni kwa njia ya simu.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alisema kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), inaunga mkono kazi za ubunifu wa kiteknolojia kwa kutoa rasilimali za mawasiliano zinazohitajika bure kwa kipindi cha miezi mitatu, ili kuwawezesha na kuinua bunifu zao.

Alisema miaka ya nyuma ilikuwa ngumu kwa wabunifu kufanya utafiti na ubunifu wao wa kiteknolojia kwa kuwa walikuwa wanalazimika kununua rasilimali za mawasiliano kama masafa, lakini kwa sasa TCRA inawezesha kutoa rasilimali hizo bila gharama yoyote kwa kipindi cha siku 90.

Aliongeza kuwa COSTECH wana mchango katika kutambua iwapo wazo hilo la kiubunifu litaleta manufaa kwa jamii endapo litapatiwa rasilimali hizo na kuendelezwa kwa ajili ya kutumia teknolojia katika kutatua changamoto mbalimbali.

Aidha, alisema pia wanatoa mwongozo ya utaratibu mzuri utakaofuatwa ili wanafunzi na wabunifu wengine waweze kunufaika na kujiendeleza kimaisha.

Dk. Jabiri aliwasihi wabunifu mbalimbali kutumia fursa hiyo kikamilifu, ili kuchochea maendeleo ya teknolojia yatakayosaidia kukuza uchumi wa kidigiti.

Wanafunzi hao walioshiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA ambayo huadhimishwa kila Alhamisi ya mwishoni mwa Aprili kwa lengo la kuhamasisha wasichana kuchukua masomo ya sayansi.

Siku hiyo inatokana na makubaliano ya nchi wanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya TEHAMA (International Telecommunications Union - ITU) kwa kauli mbiu ya maadhimisho hayo mwaka 2024 ni "Uongozi".

# EPZA yahimiza uwekezaji uchakataji korosho

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji na Mauzo nje ya Nchi (EPZA), imewataka wawekezaji wa ndani na nje kuchangamkia fursa kubwa katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na korosho kwa ajili ya kuuza nje ya nchi na kuchangia pato la taifa na uchumi wa nchi.

Tanzania inasifika kwa kuwa na korosho nzuri duniani ambazo zinawahakikishia wawekezaji kupata soko la uhakika kimataifa hasa zinapoongezwa thamani.

Tanzania imeweka mkakati wa kuongeza uzalishaji wa korosho hadi kufika tani milioni moja ifikapo mwaka 2030, mpango ambao utaongeza uchangiaji wa sekta ya kilimo katika uchumi wa nchi.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, alisema hayo wakati walipotembelea kiwanda cha kuchakata korosho cha Tan Ko Mirae Green Company kutoka Korea kilichopo wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani kuwa kuna fursa kubwa katika uchakataji wa korosho ambao unamhakikishia mwekezaji kupata faida kubwa.

"Nawahimiza wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika uchakataji wa korosho hasa kupitia Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ) na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya (SEZ) kwani yanawapa uhakika wa kupata faida kubwa," alisema.

Alisema katika ziara hiyo walitembelea viwanda sita katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani hasa Wilaya ya Mkuranga ikiwa ni mwendelezo wa kukagua na kufanya tathmini ya viwanda ambavyo vimepewa leseni na EPZA zaidi ya 200 nchini.

Maziku alisema mamlaka ya EPZA huvutia na kusajili viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa kwa mauzo nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni katika nchi huku ikichangia kuongeza ajira, teknolojia mpya na kuhakikisha kuwa bidhaa za mazao haziuzwi nje zikiwa ghafi.

Meneja wa Uendeshaji wa Kiwanda cha Tan-Ko Mirae Green, Eric Nkanda, alisema kuwa kiwanda hicho hadi sasa kimeajiri wafanyakazi 45 na pia kinachangia kipato kwa kiasi kikubwa kwa wakulima wa korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara na wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

Hata hivyo, Nkanda alisema mgawo wa umeme ni tatizo kubwa na kuongeza gharama za uzalishaji kutokana na matumizi ya mafuta kwenye majenereta.

Kiwanda cha kuchakata korosho cha Tan Ko Mirae Green Company ambacho uwekezaji wake ni zaidi ya Dola za Kimarekani milioni tano, kilizinduliwa mwezi Desemba, mwaka jana kikiwa na uwezo wa kuchakata kati ya tani 3,000 na 4,000 za korosho kwa mwaka.

Pia, kiwanda huzalisha mafuta maalum mazito ambayo ni rafiki kwa mazingira kwa ajili ya matumizi kwenye mitambo ambayo yote soko lake lipo nchini Korea.

Kiwanda pia huzalisha kati ya tani 2,500 hadi 3,000 za mkaa kwa mwaka pamoja na bidhaa za mbolea.

Katika ziara hiyo, Mamlaka ya EPZA ilitembelea kiwanda cha kuchakata chupa tupu cha plastiki, LVDI International Enterprise Limited kilichopo Temeke, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Wang Lingang, alisema hadi sasa kimeajiri watu 85 kwa mikataba na vibarua 54.

Alisema soko lao kubwa la bidhaa zinazotengenezwa na kiwanda hicho ni pamoja na kamba za plastiki ambazo husafirishwa China, Amerika, Urusi, Korea na Vietnam.

# Jela maisha kunajisi mtoto wa miaka minne

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

FADHILI Shaibu (36), mkazi wa kijiji cha Chiwale wilayani Masasi, mkoani Mtwara amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumnajisi mtoto wa kike wa kaka yake mwenye umri wa miaka minne, baada ya kumrubuni kuwa atampa machungwa.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki mjini Masasi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Masasi, Batista Kashusha, baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote na kujiridhisha na vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa mahakamani na upande wa Jamhuri pamoja na upande wa mashtaka.

Akisoma hukumu hiyo, Kashusha alisema kuwa kesi hiyo namba 93 ya mwaka 2023 ilikuwa na mashahidi watano, na kwamba mahakama imemtia hatiani mshtakiwa kwa kumhukumu kifungo cha maisha jela baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo.

Ilidaiwa mahakamani humo kuwa mshtakiwa alifanya kosa la kumnajisi mtoto wa kaka yake Agosti 25, mwaka 2023 majira ya saa 9:30 jioni wakati akiwa nyumbani kwake katika Kijiji cha Chiwale, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na kumsababishia maumivu makali na kumharibu sehemu za siri.

Kabla ya hukumu hiyo, Hakimu alisoma maelezo ya awali akieleza kuwa siku ya tukio alifika nyumbani kwa mtoto na kumkuta mama wa mtoto ambaye ni shemeji yake akiwa na mtoto huyo ndipo alipomchukua na kuondoka naye akidai kuwa anakwenda kumnunulia machungwa kwa madai kwamba mara kwa mara alikuwa akimwomba amnunulie machungwa.

Hakimu Batista alisema mshtakiwa alipofika nyumbani kwake majira ya saa 9:30 alasiri aliingia naye chumbani kwake na kuanza kumnajisi mtoto huyo na mtoto akiporudi nyumbani alimwelezea mama yake kitendo alichofanyiwa na mshtakiwa ambaye ni baba yake mdogo.

Alisema hukumu hiyo imezingatia vipengele vyote vya msingi vya kisheria ikiwa ni pamoja na ushahidi wa kitabibu uliotolewa na daktari aliyemfanyia vipimo vyote mtoto aliyefanyiwa tukio hilo pia ushahidi mwingine ulitolewa na mama mzazi wa mtoto na mtoto mwenyewe na kwamba kwa ushahidi huo mahakama imetoa kifungo hicho kwa mshtakiwa pasipo na shaka yoyote.

Katika maelezo ya awali, Mkuu wa Mashtaka Wilaya ya Masasi ambaye ni wakili wa serikali mwandamizi Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP) Wilaya ya Masasi, Miraji Kajieuli, aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine wanaofanya vitendo kama hivyo vya kinyama.

Wakili Kajieuli alisema mshtakiwa alipaswa kuwa mlezi mwema kwa mtoto huyo na wengine walioopo katika jamii, lakini amegeuka na kuwa mnyama na kumnajisi mtoto jambo ambalo amemsababishia athari za kimwili na kisaikolojia.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri watahiniwa kidato cha sita

**JANA** wanafunzi wa Kidato cha Sita, wameanza mitihani yao na matarajio ya wengi wakiwamo wazazi wao ni kuona wanafanya vizuri ili waweze kupata alama nzuri na kuchaguliwa kujiunga na elimu ya juu.

Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), juzi lilitangaza kuanza kwa mitihani hiyo ambayo ilianza jana na kutarajiwa kumalizika Mei 24.

Ni matumaini ya wazazi wengi kuwa watahiniwa hao wamejiandaa vizuri ni mitihani ili kuepuka aibu ambayo imejitokeza miaka ya nyuma yakuandika mambo yasiyofaa.

Mitihani ni kipimo cha wanafunzi kuona yale waliyofundishwa na walimu wao yamewaingia vizuri ili hata wanapochaguliwa kwenye kujiunga na elimu ya juu au vyuo vingine sawa na hivyo wanafanya vizuri.

Kwa mujibu wa NECTA wahiniwa 113,504, wamesajiliwa kufanya mitihani ya kidato cha sita mwaka huu na kati yao watahimiwa 104,449 ni wa shule na 9,055 ni wa kujitegemea.

Idadi ya watahiniwa ni kubwa na kila mmoja anatarajia anapomaliza apate alama nzuri ili aweze kujiunga na elimu ya juu.

Elimu ndio msingi wa maisha, bila kuwa na elimu nzuri baadhi ya mambo yanakwama kwa sababu ya kukosa mwongozo mzuri.

Tanzania kwa sasa ina vyuo vingi vya elimu ya juu hali inayowawezesha watahiniwa wengi kupata fursa ya kujiunga navyo.

Tofauti ni miaka ya nyuma, chuo kilichokuwa kikitegemewa sana ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho ni chuo cha serikali, lakini kwa sasa kuna vyuo vingi vya elimu ya juu kwenye baadhi ya mikoa.

Mbali na vyuo hivyo, pia kuna vyuo vya ufundi ambavyo vimewasaidia wanafunzi wengi wanaosoma kwenye vyuo kutoka wakiwa na utalaamu na kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira za serikalini.

Vyuo vimewasaidia wanafunzi wengi kujiendesha kimaisha kutokana na kupata elimu nzuri ya kuwasimamia wanapoanza jambo lolote linalohusu kujiajiri.

Sasa kuna wanafunzi wengi waliomaliza vyuo vya elimu ya juu ambao walisomea fani nyingine, lakini baada ya kukosa ajira serikalini, wameamua kuanzisha biashara zao na mambo yao yamekwenda vizuri baada ya kupata mwongozo.

Tofauti na miaka ya nyuma hivi sasa vijana wengi wanachakarika kujiajiri wenyewe na wengine kufanikiwa kufanya vizuri na kuajiri wenzao.

Hata Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akitoa salamu kwa watahiniwa hao amesema anatarajia kuona vipwa, juhudi na kujituma ili kuleta mchango wao katika maendeleo ya nchi siku zijazo.

Aliwaahidi kuwa ataendelea kufanyakazi, kupanga na kutekeleza mipango na sera zitakazowawezesha kutumiza nia ya kuwa na wananchi wenye mchango mkubwa kwa jamii na taifa.

Amewaahidi kuongeza fungu kwa wanafunzi zaidi kupata mikopo ya elimu ya juu na kuboresha sera na mazingira ya kukua kwa sekta binafsi ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha ajira nchini.

Amewaombea watahiniwa kwa Mwenyezi Mungu wafanikishe katika hatua hiyo kwa mafanikio na kila jema katika hatua zinazofuata.

Rais wa nchi anapotumia muda wake kuwaombea watahiniwa ni jambo kubwa ambalo wanatakiwa kulichukulia kwa uzito ili wasimwangushe matokeo yanapotoka.

Ametoa ahadi nyingi ikiwa kuongeza bajeti kwenye Wizara ya Elimu, ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Mitihani kidato cha sita chonde chonde udanganyifu

**WANAFUNZI** wa kidato cha sita, walianza mtihani wao jana, huku watahiniwa hao 13,504 wakiwamo wa ualimu ngazi ya cheti na stashahada nao wakitarajiwa kufanya mtihani wao.

Wakati wakiendelea na mitihani, si vibaya kuendelea kukumbusha kuwa vitendo vya udanganyifu ambavyo vimekuwa vikifanyika kwenye mitihani hiyo vinachangia kuporomosha elimu.

Kila mwaka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), linapotangaza matokeo ya mtihani, huwa kuna taarifa ya kuwafutia matokeo baadhi ya wanafunzi kwa sababu za kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo.

Mfano, katika matokeo ya mitihani ya kidato cha sita ya mwaka 2023/2024, watahiniwa 11 walifutiwa matokeo baada ya kubainika kufanya udanganyifu katika mtihani huo.

Hayo ni kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed. Hivyo ingekuwa ni vyema udanganyifu huo usiendelee kujitokeza katika mitihani ya mwaka huu, ili kulinda hadhi ya elimu.

Ninaamini kwamba udanganyifu wa mitihani ukidhibitiwa mitihani tutaokoa elimu yetu, kwani tabia ya wizi na udanganyifu wa mitihani limekuwa kama jambo la kawaida na kumbe elimu inakufa.

Inakufa kwa maana gani? Kwa sababu wizi ukiendelea, mwisho wake nchi itajikuta haina wasomi mahiri ambao wanafaa kuwa wataalamu bora wa fani mbalimbali hapo baadaye.

Wakati serikali ikipanga na kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya maendeleo, ni muhimu kukumbushana umuhimu wa elimu katika kuchochea maendeleo ya sekta nyingine zote.

Udanganyifu au wizi wa mitihani sio sifa njema kwa taifa kwani unachangia kuporomosha taifa kielimu, hivyo ni vyema wadau wote wa elimu kukemea na kutoshiriki vitendo hivyo.

Ni aibu kuona wanafunzi wanafaulu na kuchaguliwa kwenda katika shule za vipaji, lakini wakifika na kufanya mitihani wakwama kupata alama za juu kutokana na kwamba walifanya wizi na udanganyifu wa mitihani.

Umefika wakati biashara ya ufaulu isiwe chachu ya wizi na udanganyifu, bali upingwe na kila mdau anayependa maendeleo ya elimu ili kuandaa wasomi bora wa baadaye watakaolisaidia taifa.

Zipo shule nyingi ambazo zinafaulisha kwa jasho na kwa mfumo wa haki, lakini pia zipo inazotumia njia ovu katika kufikia ufaulu huo ili kuvutia biashara, lakini mwisho wake ni kupata wasomi wasio na sifa.

Biashara ya ufaulu kwa njia ovu zinazotumiwa kama nyenzo au ngazi ya kumvukisha mwanafunzi kutoka daraja moja hadi jingine, kimasomo bila kujali ufahamu au uelewa wake ni hatari kwa maendeleo ya elimu.

Hivyo, kwa mchezo huu ni sawa na kuchimbia kaburi elimu yetu, taaluma ya watoto wetu na hatimaye kubakia na taifa la watu wenye ukosefu wa fikra, weledi, ujuzi na ufahamu katika mambo mbalimbali.

Katika kufanikisha vita dhidi ya vitendo hivyo, kuna haja ya kuwa na mikakati endelevu la kufuatilia hao wanaodaiwa kufanya vizuri katika mitihani ya juu ili kujua ufaulu wao tangu chini.

Njia hiyo kwa namna moja au nyingine, inaweza kusaidia kuwabaini na hata kupata wale wanaowasaidia katika udanganyifu na kuwasaidia kupata ufaulu wa juu huku wakiwa na uwezo mdogo darasani.

Maisha ya shule ni safari ndefu yenye milima na mabonde, hivyo ni muhimu mwanafunzi ajitahidi kusoma kwa bidii ili aweze kufaulu, sio kusubiri njia mbadala ya kufaulu, yaani wizi na udanganyifu.

Niwatakie kila heri wanafunzi wa kidato cha sita walioanza mitihani yao jana, lakini wasikubali kuingizwa katika mchezo wa kuiba au kufanya udanganyifu wa aina yoyote, bali watumie uwezo wao wa darasani kulingana na jinsi walivyofundishwa na walimu wao.

# DC Ilala awahakikishia wananchi nishati safi

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amesema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi wanahakikisha wanatimiza lengo la maendeleo endelevu kwa kila Mtanzania kupata nishati endelevu, safi na nafuu ifikapo mwaka 2030.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya utunzaji wa mazingira itakayoendeshwa na Kampuni ya Watu Credit (Tanzania) ambao wana mpango wa kufadhili madereva wa bajaji zinazotumia gesi asilia zaidi ya 1,000 ifikapo mwisho wa mwaka 2024.

Alisema kampeni hiyo imekuja wakati kukiwa na dhamira ya kukuza matumizi ya vyombo vya moto vinavyoendeshwa kwa kutumia gesi asilia (CNG) pamoja na vinavyotumia umeme.

"Tupo hapa leo (jana) kudumisha dhamira yetu ya wazi ya kukuza matumizi ya magari ya miguu mitatu (bajaji) yanayoendeshwa kwa gesi asilia (CNG) na hata yale yanayotumia umeme na hivyo kupunguza utegemezi wa mafuta yanayosababisha ongezeko la hewa ukaa iletayo ongezeko la joto duniani huku sekta ya usafirishaji ikichangia kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa mazingira," alisema Mpogolo.

Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya Watu Credit (Tanzania), Rumisho Shikonyi alisema; "Kuhamia kwenye nishati safi ni muhimu, na tumejitolea kufadhili mpango huu ili kuwasaidia abiria, madereva na jamii kutumia usafiri safi, salama, na endelevu. Hii itatusaidia kulinda mazingira yetu kwa sababu mustakabali wa sayari yetu yote unategemea hatua tunazochukua leo," alisema.

Alisema kampuni hiyo imekuwa ikifanya kazi lengo la utunzaji wa mazingira na katika kipindi cha miezi miwili wamefadhili zaidi ya bajaji 200 zinazoendeshwa kwa gesi asilia zenye thamani ya Sh. bilioni 2.2.



Mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan, alitangaza kampeni ya kuwezesha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa asilimia 80 ili kuwaondoa kwenye kero wanawake hasa waishio vijijini.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), Asma Mwinyi (kushoto), akifurahi na wanafunzi baada ya kuwapatia msaada wa taulo za kujisitiri wakati wa hedhi visiwani Pemba jana. Taasisi hiyo hadi sasa imewafikia wanafunzi 30,000 Bara na Visiwani lengo likiwa ni kuwasaidia wasikose masomo wakiwa katika hali hiyo. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Matarajio ya Samia watahiniwa kidato VI

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaeleza watahiniwa wa kidato cha sita walioanza mitihani yao jana kuwa, anatarajia kuona vipawa, juhudi na kujituma ili kuleta mchango wao katika maendeleo ya nchi siku zijazo.

Katika ukurasa wake wa Instagramu, Rais Samia alitoa ahadi yake kwa wanafunzi hao kuwa ataendelea kufanyakazi, kupanga na kutekeleza mipango na sera

zitakazowawezesha kutimiza nia ya kuwa na wananchi wenye mchango mkubwa kwa jamii na taifa.

"Ikiwamo kuongeza fungu kwa wanafunzi zaidi kupata mikopo ya elimu ya juu na kuboresha sera na mazingira ya kukua kwa sekta binafsi ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha ajira nchini," alisema Rais Samia katika ukurasa huo.

Aidha, aliwaombea watahiniwa kwa Mwenyezi Mungu wafanikishe katika hatua hiyo kwa mafanikio na kila jema katika hatua zinazofuata.

"Nina imani kuwa mmetumia muda wenu shuleni kujiandaa vyema, hasa baada ya serikali kuamua kufuta ada kwa kidato cha kwanza hadi sita, kujenga na kuboresha shule zaidi.

"Ujenzi wa mabweni sehemu ambazo wanafunzi hasa wa kike walikuwa kwenye mazingira hatarishi na kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Uamuzi huu umeleta nafuu na faraja katika familia nyingi na ongezeko la watahiniwa zaidi kutoka 106,883 mwaka 2023 hadi 113,504 mnaoanza mitihani leo (jana), alisema.

Juzi Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed, alitangaza kuanza kwa mitihani ya kidato cha sita kuanzia jana hadi Mei 24, 2024 na ualimu itakayomalizika Mei 20.

Katika mitihani hiyo watahiniwa wa shule waliosajiliwa, wavulana ni 57,378 sawa na asilimia 54.9 na wasichana ni 47,071 sawa na asilimia 45.1.


Watahiniwa wenye mahitaji maalum ni 232 na kati yao, 201 ni wenye uoni hafifu, 16 ni wasioona na 15 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili.

Aidha, kati ya watahiniwa wa kujitegemea 9,055 waliosajiliwa, wavulana ni 5,515 sawa na asilimia 60.91 na wasichana ni 3,540 sawa na asilimia 39.09.

Watahiniwa wa kujitegemea wenye mahitaji maalum wako watatu ambao wote ni wenye uoni hafifu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wataalamu wa miwa waishauri serikali kuboresha utafiti

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

WATAALAMU wa miwa na sukari Tanzania wameishauri serikali kuendelea kuboresha huduma za utafiti na mazingira ya uwekezaji ili kufikia lengo la uzalishaji wa sukari nchini kutokana na sekta hiyo kukabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa uhakika wa mbegu za miwa zinazofaa kwa uzalishaji wa sukari.

Hali hiyo inatajwa kuwa ni changamoto kubwa licha ya jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na serikali katika kukabiliana na changamoto za sekta hiyo ikiwamo bei na upatikanaji wa uhakika kutokana na karibu asilimia 90 ya mbegu zinazofaa kuzalisha miwa inayofaa kwa sukari kuagizwa nje ya nchi.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Chama cha Wataalamu wa Miwa na Sukari Tanzania (TSCCT), Fedrick Charles, alisema hayo kwenye kongamano la 10 linalokutanisha wataalamu mbalimbali wa sekta hiyo kutoka viwanda vyote vya sukari nchini ikiwamo Kilombero Sugar, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, TPC, Mkulazi Holding Company, Bagamoyo Sugar na taasisi nyingine zote zinazojihusisha na sekta hiyo.

Alisema ukosefu wa mbegu za kisasa zenye kiwango kikubwa cha sukari unasababisha wamiliki wa viwanda kuagiza mbegu hiyo nje ya nchi hasa katika nchi za Afrika ya Kusini, Mauritius, Malawi na nchi zingine.

Alisema ili kuongeza tija mashambani na utoshelevu wa sukari nchini ipo haja ya kuwa na maabara ya kutafiti kwa ajili ya kuangalia afua ya udongo, viatilifu na mbegu zinazoendana na ikolojia.

Changamo nyingine walizozibainisha wataalamu hao wa sukari ni ukosefu wa mashine mbalimbali za viwandani na zinazo sababisha pia kuagizwa nje ya nchi na kuongeza gharama za uzalishaji hali inayopandisha bei ya sukari pamoja na maabara ya kufanya uzalishaji wa mbegu 'planting breeding'.

"Ndio maana tunawasihi wadau mbalimbali wa sekta ya sukari kuona fursa ya uwekezaji wa vifaa hivyo hapa nchini kutokana na uhitaji wake kuendelea kukua siku baada ya siku, lakini ili kuwe na kilimo endelevu cha miwa ya sukari inahitajika teknolojia ya kisasa ya umwagiliaji na uvunaji wa kutumia mashine za kisasa," alisema.

Hata hivyo, alisema bado nchi imeendelea kufanya jitihada mbalimbali kukabiliana na changamoto katika sekta ya miwa na sukari ikiwamo kuwekeza kupata wataalamu wengi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, George Gowele, alisema mikakati mbalimbali inayoendelea kufanywa na serikali ili kuondoa changamoto hiyo ya mbegu ikiwamo jitihada kubwa kupitia Wizara ya Kilimo na Taasisi ya Utafiti wa Mbegu nchini TARI kituo cha Kibaha ili kuendana na uhitaji.

Alisema jitihada hizo zimeanza muda mrefu tangu mwaka 2005 na tayari kuna mbegu ambazo tayari zimeandaliwa ikiwamo aina ya Tariska 121-122 ambazo tayari zimeanza kuoteshwa kwa majaribio katika maeneo mbalimbali.

Jitihada zingine ni uanzishwaji wa vitalu vya mbegu katika kiwamda cha Sukari Mtibwa kwaajili ya wakulima wadogo na Mkoa wa Manyara vitakuwapo vitalu kwa lengo la kuondoa changamoto ya mbegu za miwa nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisisitiza wataalamu hao kutambua kuwa wao ni jicho la taifa katika sekta ya sukari na lazima waweke nguvu kuondoa changamoto zilizopo.

Alitoa wa mfano hali iliyopo sasa ya mabadiliko ya hali ya hewa na namna yanavyoathiri ukuaji wa sekta hiyo na kwamba ni vyema kuwa wabunifu na kutumia teknolojia za kisasa ili kwenda sambamba na malengo ya nchi.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC wakiwa na tuzo yao waliojishindia baada ya kampuni hiyo kuibuka kinara kwenye tuzo za usalama mahali pa kazi, kundi la Tehama katika maonyesho yaliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) mkoani Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: BADI JOHN**

# Mtambi awaonya watumishi wazembe, wabadhirifu

**Na Samson Chacha**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Evance Mtambi, amewaonya watumishi wa umma wazembe kazini wakati wa kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, amewaonya kutohujumu fedha za miradi ya maendeleo na kuwataka kufanya kazi kwa uadilifu na kuepuka vitendo vya rushwa.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake wilayani Tarime, soko jipya linalojengwa akiongozana na Mkuu wa wilaya hiyo, Kanali Maulid Surumbu, wenyeviti wa halmashauri za Tarime mji, Daniel Komote, Saimon Kles wa Tarime Vijijini na wakurugenzi wa halmashauri hizo, Gwimbana Ntovya na Solomon Shati kamati za ulinzi mkoa na Wilaya Tarime.

Kanali Mtambi alisema atawashughulikia watumishi wazembe kazini, wala rushwa, wanaohujumu fedha za miradi ya maendeleo inayoletwa na serikali ikiwamo ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, madarasa, barabara, maji na watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu wa mali ya umma atawakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

"Soko hili la Tarime limechukua muda kukamilika mnadai kuna changamoto zilikuwapo za upatikanaji wa kokoto mara mvua na malipo kwa mkandarasi zaidi ya bilioni moja serikali ilishatoa fedha za mradi huu wa kukamilisha soko hili na kwa mkandarasi ahakikishe majengo ya soko hili linajengwa kwa viwango vilivyotakiwa na vipimo sahihi bila kuhujumiwa.

"Huko Tarime Vijijini nimepita Kata ya Mriba, Tarafa ya Ingwe ninaambiwa kuna utoro wanafunzi zaidi ya 40 wa kike wameshindwa kuhudhuria masomo bila sababu na baadhi yao huenda wametoroshwa, wazazi, walimu na uongozi wa kata na tarafa wanatakiwa kufuatilia utoro huo ili wahusika waliowatorosha wanafunzi hao kuchukuliwa hatua za kisheria," alisema Mtambi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime Mji, Gwimbana Ntovya, alisema kuwa 'Soko jipya la Tarime ujenzi umefikia asilimia 87 bado ukamilishaji wa milango na sehemu ya mbele yenye vibanda 325 vya maduka, vidimba 160, bucha tatu, migahawa miwili, super market moja, benki mbili na kukamilika kwa soko hilo kutasaidia kukusanya mapato ya zaidi ya Sh. milioni 588 kwa mwezi fedha ambazo zitasaidia katika ujenzi wa miradi ya umma katika halmashauri.

# Wagonjwa moyo Sierra Leone kutibiwa JKCI

**Na Joseph Mwendapole**

UJUMBE wa wataalamu wa Wizara ya Afya kutoka Sierra Leone, wameingia makubaliano na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kwa ajili ya kutibu wagonjwa wanaotoka nchini humo.

Wataalamu hao walikuja nchini mwishoni mwa wiki kujifunza namna ya kuanzisha matibabu ya moyo nchini kwao huku wakishangaa uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali, Taasisi ya JKCI.

Akizungumza wakati wa kupokea ujumbe huo, Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema ziara hiyo inalenga kuendeleza ushirikiano wa matibabu ya moyo kati ya Tanzania na Sierra Leone ikiwa ni dhamira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kutangaza utalii tiba kimataifa.

"Ujumbe huu umefika hapa nchini kujifunza uwekezaji wa matibabu ya moyo na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kutoka kwa Bohari ya Dawa (MSD), ikiwa ni uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ya Rais Dk. Samia," alisema Dk. Kisenge.

Alisema ujumbe huo wa wataalamu kutoka Sierra Leone umekiri kujifunza mambo mengi kutoka JKCI na wataleta wagonjwa na wao kwenda kuanzisha taasisi yao kwa ushirikiano na taasisi ya JKCI.

Dk. Kisenge alisema wataalamu hao wa Sierra Leone, wamejifunza utendaji kazi mkubwa na imara kutoka kwa watumishi wa JKCI, ikiwamo namna ya kuhudumia wagonjwa mahututi.

Alisema kuwa ugeni huo ni hatua kubwa ambayo inatimiza malengo ya Rais Dk. Samia ya kukuza tiba utalii nchini kutokana na uwekezaji mkubwa alioufanya kwenye sekta ya afya.

Aliongeza kuwa, mbali na huduma za upasuaji wanazofanya hospitalini hapo, wanaendelea kutoa huduma za upimaji wa moyo kupitia mpango wao wa Dk. Samia, Tiba Mkoba.

Alisema mpango huo unasogeza huduma hizo karibu na wananchi huku wakizijengea uwezo hospitali zingine za kanda ikiwamo Benjamin Mkapa pia Chato na Geita.

Naye Mganga Mkuu wa Siera Leone, Sertie Kenneh, ambaye ni kiongozi wa msafara huo alisema, amefurahi kufika JKCI na kujifunza kazi kubwa ya matibabu ya moyo wanayoifanya kwa kuwa na uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba.

Aliipongeza serikali kwa uwekezaji mkubwa iliyofanya JKCI kwa kuwezesha matibabu ya magonjwa kwa wananchi kutoka nchi mbalimbali za Afrika huku wakiahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kuanzisha matibabu hayo.

"Tumejifunza vitu vingi namna ya utoaji huduma bora za matibabu kwa wagonjwa, ushirikiano uliopo baina ya watumishi wa taasisi ya JKCI kufanikisha lengo la huduma bora, hivyo nasisi tutaendelea kuimarisha ushirikiano," alisema.

Alisema kutokana na ubora wa huduma walizoziona JKCI nchi yao italeta wagonjwa wao kutibiwa hapo ili kupunguza gharama za kusafirisha wagonjwa kwenda Ulaya na India.

Naye Mkurugenzi wa Tiba Shirikishi wa JKCI, Dk. Delila Kimambo, alisema mafanikio ya taasisi hiyo yanatokana na ushirikiano mkubwa walio nao watumishi wa taasisi hiyo.

"Mafanikio haya yanayoonekana kwa ubora mkubwa katika kutoa matibabu siyo ya jitihada za mtu mmoja, bali yanatokana na ushirikiano wa watumishi wote kuhakikisha tunafikia lengo lililokusudiwa," alisema.

Alisema wataendelea kuimarisha ushirikiano na mataifa mbalimbali kuwavutia ili kuleta wagonjwa kutibiwa katika taasisi hiyo.



# Awesu atangaza neema ya maji vijiji 2,500

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema visima 900 vitajengwa katika vijiji 2,500 nchini ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji.

Aweso alitangaza neema hiyo jana wakati akizindua programu maalumu ya uchimbaji wa visima hivyo katika Kata ya Measkron na Dawari Wilaya ya Hanang' mkoani hapa.

Alisema kati ya vijiji 12,318 vilivyopo nchini, 9,737 vimepelekewa huduma hiyo na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Alisema wizara hiyo, ilifanya tathmini na kubaini upatikanaji wa maji kwa mjini kwa sasa ni asilimia 90 na kwa vijijini 79.6.

Awesu, alisema wizara hiyo imeamua kuzindua mradi huo Manyara kwa kuwa kipindi cha mafuriko yaliyotokea Hanang' walikuwa wakitumia siku moja kuchimba kisima badala ya siku 21.

"Zaidi ya Sh. bilioni 40 tumepewa ili tukachimbe visima 900 nchi nzima, hatutachimba visima na kuondoka, bali tutajenga na miundombinu ili watu wapate maji," alisisitiza Aweso.

Aliitaka Hanang' iwe ya kwanza kukamilisha mradi na kuonya asije kutokea mhandisi akakwamisha jitihada za serikali za kuwapelekea huduma hiyo wananchi.

Vilevile, alitoa siri ya Manyara kuwa wanaofanya miradi kusimamiwa kwa umakini, kujengwa kwa ubora na kubakiza fedha kiasi cha Sh. milioni 200 kwa mradi mmoja ni Meneja wa RUWASA wa Mkoa huo, Wolter Kirita na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mji wa Babati (BAWASA), Iddy Msuya.

Aweso, alisema uadilifu wa viongozi hao wa maji unasaidia wizara yake kukamilisha miradi kwa wakati na kuwa na ubora.

Awali, Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, alisema mwaka 2021 upatikanaji maji salama kwa Manyara ulikuwa asilimia 55.8 kwa sasa umeongezeka hadi asilimia 70.5.

"Sisi kama mkoa tunapokea visima 30 vitakavyojengwa Manyara ila havitutoshi tunaomba utuletee vingine na tuko tayari kuvitunza," alisema Sendiga.

Aliungana na Waziri Awesu kuwa Meneja wa RUWASA Manyara na Mkurugenzi wa BAWASA wanasimamia vizuri miradi ya maji na kuwa na ufanisi.

Alisema miradi ya BAWASA anadhani imesimamiwa na kampuni za kigeni kutokana na ubora wake.

Machi 15, mwaka huu, Kirita akiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya taasisi yake kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alisema mpango wa serikali kupeleka maji vijiji vyote kupitia programu maalumu, utaanza na mikoa mitano, ukiwamo Manyara.

Alitaja miongoni mwa vigezo vilivyoupa mkoa huo miradi hiyo kuwa ni kijiji kisiwe na huduma, kijiji kisiwe mjini na vijiji vilivyo barabara kuu vitapewa kipaumbele.

Vilevile alitaja mikoa ya kwanza itakayonufaika kuwa ni Manyara kutokana na maafa yaliyotokea hivi karibuni Hanang', Arusha, Lindi, Mbeya na Njombe.

## Gambo akabidhi magari ya wagonjwa

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo amekabidhi magari mawili ya kubebea wagonjwa kwa Kituo cha Afya cha Muriet na Hospitali ya Rufani ya Mtakatifu Meru.

Gambo amekabidhi magari hayo mwishoni mwa wiki iliyopita akiwa ziarani katika Kata ya Muriet kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi, akiwa ameambatana na wataalamu wa Mkoa wa Arusha.

"Serikali inatoa bure magari haya hata wagonjwa hawatakiwi kulipia gharama wanapolazimika kutumia magari haya," alisema.

Gambo aliwataka wananchi kuwasilisha matatizo yanayowakabili na kuwaahidi kuyatatua.

Wakitoa kero zao, wakazi wa Muriet, walisema ubovu wa barabara nyingi katika kata yao unakwamisha maendeleo na kuiomba serikali kuwapatia vivuko vinavyounganisha barabara mbalimbali.

Dickson Mahenge, alisema ujenzi wa miundombinu ya soko la kwa Morombo bado umebaki kama agenda iliyokufa.

"Tunalipishwa ushuru Jumatatu hadi Jumapili ambayo ni siku ya mapumziko, lakini halmashauri haituangalii ikatujengea soko, na hela zetu wanachukua kila siku wana maana gani, tunanyeshewa, tunapigwa jua na upepo," alisema Mahenge.



Diwani wa Kata ya Loiborsiret wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Ezekiel Lesenga (Maridadi), akizungumza kwenye kikao cha kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero na changamoto za wakazi wa kijiji cha Loiborsiret juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Bidhaa za ngozi zaongezwa thamani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MRATIBU wa Kitaifa wa shirika lisilo la kiserikali la Solidaridad nchini, Mary Mkonyi amesema wameongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa za ngozi kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini.

Mary alisema hayo jana jijini hapa wakati wa kikao kazi cha wadau wa shirika hilo cha kupitia utekelezaji wa mpango wa usaidizi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa maendeleo ya viwanda na sekta za uzalishaji (SIPS).

Alisema mpango huo wa miaka mitano ulianza kutekelezwa mwaka 2019 na kuratibiwa na Sekretarieti ya SADC na kufadhiliwa Euro milioni 18 na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya Mfuko wa 11 wa Maendeleo ya Ulaya (EDF).

Alisema mpango huo umejumuisha mradi wa miaka miwili wa kuimarisha mnyororo wa thamani wa bidhaa za ngozi katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na Kusini.

"Mpango wa kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya ngozi kwa kuwawezesha ujuzi wajasiriamali wanaozalisha bidhaa za ngozi nchini, ulianza Februari mwaka 2022 na unahitimishwa mwezi huu, umepata mafanikio makubwa. Watengenezaji wa bidhaa za ngozi wamepata fursa ya ujuzi kupitia kituo chetu kilichoko Moshi mkoani Kilimanjaro," alisema Mary.

Alisema kituo hicho kinaweza kutumiwa na wajasirimali nchini wanaojihusisha na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa kupata teknolojia za kisasa ambayo inaongeza ufanisi na kuokoa muda waliokuwa wanatumia.

Mwandamizi wa Programu za Solidaridad Tanzania, Godlove Nderingo, alisema wameimarisha ushirikiano kati yao na serikali kwa kuunganisha wadau ili kuongeza ubora wa bidhaa za ngozi.

"Katika programu hii ya kuongeza thamani mazao ya ngozi tumeshirikiana na Chama cha Ngozi Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), na viwanda vya ngozi vya ndani," alisema.

Humphrey Nxumalo, Mkuu wa Mipango wa Solidaridad Kusini mwa Afrika, alisema mradi kama huo umetekelezwa nchini Zimbabwe kwa kipindi hicho.

"Mradi huu wa kukuza sekta ya ngozi una ushindani mkubwa na tumelenga kukuza ufumbuzi wa ubunifu katika sekta ya ngozi na kuunda uhusiano wa soko kwa bidhaa za ngozi ndani ya nchi, kikanda na kimataifa," alisema.

Alisema wameboresha uwezo wa kubuni bidhaa za ngozi kwa kuanzisha studio za Usanifu Bora Tanzania na Zimbabwe na kutolea mfano bidhaa za ngozi awali ambazo zilichukua wiki kusanifu na kwa sasa zinaweza kukamilika kwa saa moja.

## Wananchi wahimizwa kutunza mazingira

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Zainab Abdallah, amewahimiza wananchi kutunza mazingira kwenye maeneo wanayoishi kwa kufanya usafi ili kukabiliana na mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza.

Akizungumza wakati akishiriki kufanya usafi kwa kushirikiana na wananchi katika Soko Kuu la Muheza na kituo cha mabasi cha Bombani, Zainabu, alisema wameweka mikakati ya kuhakikisha mji wa Muheza unakuwa safi.

" Tumeweka mikakati ya kuhakikisha mji wa Muheza unakuwa safi na salama na sheria inaendelea pale pale kwa wachafuzi wa mazingira kuhukumiwa kifungo ama faini, " alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Aliwashukuru vijana kwa kuitikia wito wa kushiriki kufanya usafi wa mazingira na mazoezi ya viungo.


"Hakika mazoezi ni afya, tunaendelea kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ili tujikinge na magonjwa yasiyoambukiza," alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mohamed Mfaki na Mkurugenzi wa Halmashauri, Jumaa Mhina kwa nyakati tofauti, walisema kampeni ya kufanya usafi katika mji huo na mazoezi ya viungoni ni endelevu ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika hatua nyingine; mkuu huyo wa wilaya alikabidhi vifaa wezeshi kwa wakulima wa mwani vilivyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian ili kuwainua kiuchumi.

Vilevile alikabidhi vyeti kwa wakufunzi wa wilaya hiyo ya Muheza walioshiriki kikamilifu katika Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika nchini mwaka 2022.

Zainabu, alitembelea Bandari ya Kigombe na Hifadhi Bahari ya Hindi Tanga Silikanti kwa ajili ya kuifungua kiuchumi na kufanya mkutano na wakazi wa Kijiji cha Msakangoto ikiwemo kutoa suluhu ya migogoro ya sugu ya mashamba ya Amboni na wafugaji.





# Mkulima jela kwa kuhujumu miundombinu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Igunga mkoani hapa, imemhukumu mkulima, Mohamed Makala (28) kifungo cha miaka 20 jela baada ya kupatikana na hatia ya kuharibu miundombinu ya maji.

Vilevile imemhukumu mkulima mwingine, Kalolo Wilbati (52) mwaka mmoja jela kwa kukutwa na vitu vya wizi mali ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Igunga (IGUWASA).

Kabla ya hukumu kutolewa, Waendesha Mashtaka wa Ofisi ya Mashtaka Wilaya ya Igunga, Grace Lwila na Albanus Ndunguru kwa nyakati tofauti, walidai mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Edda Kahindi kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Machi 2 na Mei 2, mwaka jana.

Lwila alidai kuwa mshtakiwa Wilbati alikutwa na vitu hivyo vya wizi zikiwamo mita za maji na mabomba ambavyo vilikuwa vimeibiwa katika maeneo mbalimbali mjini Igunga.

Alidai mshtakiwa Makala anadaiwa kwa makosa matatu ya kuingilia miundombinu ya mifumo ya maji ya IGUWASA na kuiba baadhi ya vifaa.

Mwendesha mashtaka huyo, aldai mshtakiwa huyo alikuwa akiiba vitu hivyo usiku kwa wateja wanaotumia maji ya IGUWASA yaliyounganishwa kutoka Ziwa Victoria na kuacha yakipotea na kuisababishia hasara zaidi ya Sh.milioni 4.4.

Aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa hao kwa kuwa serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa kuwekeza sekta ya maji nchini.

Baada ya kusikiliza mashahidi saba wa upande wa mashtaka na utetezi, Hakimu Kahindi alitoa hukumu dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya kuhujumu miundombinu ya maji na kuisababishia serikali hasara.

Hakimu Kahindi alisema mshtakiwa Wilbati atatumikia kifungo cha mwaka mmoja jela baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na vitu vya wizi.

Alisema mshtakiwa Makala atatumikia kifungo cha miaka 20 jela baada ya kupatikana na hatia ya makosa matatu.



Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi mkoa wa Shinyanga, Monica Sehere, akitoa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wananchi wa Nyamalogo wilayani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Jamii yahimizwa kutunza mazingira

**Na Remmy Moka,** SAUT

JAMII imetakiwa kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na magonjwa ya mlipuko na kumbukiza kutokana na uchafu.

Rai hiyo ilitolewa na Meneja Mradi wa Taasisi ya Synergistic Globe, Erick Kafuluki, wakati wa utoaji elimu kwa kushirikiana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) Mwanza Kituvo cha Mawasiliano ya Umma wakati walipotembelea Ofisi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Sweya iliyopo Kata ya Luchelele Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza.

Kafuruki, alisema lengo la kutoa elimu kwa mabalozi wa Mtaa wa Sweya ni kuhakikisha wanahimiza wananchi kuweka maeneo yao katika hali ya usafi na kuepuka na magonjwa ya mlipuko na kuambukizwa kutokana na uchafu.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Bahati Alfonce, alisema hauna mawakala wa usafi, hivyo taasisi hiyo imekuja na mpango kazi wa kusaidia kuboresha usafi katika mtaa wao.

Balozi Witness Chacha wa shina namba nne katika mtaa huo, alitoa wito kwa taasisi hiyo kuweka gharama nafuu kulingana vipato vya wananchi.

## Huduma kliniki tembezi mwarobaini wajawazito kujifungulia nyumbani

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

UANZISHWAJI wa huduma ya Kliniki Tembezi katika Kata ya Mwamala Halmashauri ya Shinyanga, umeondoa dhana potofu kwa wajawazito kujifungulia nyumbani na kushindwa kuhudhuria kliniki na kunusuru vifo mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mwamala, Dk. Dioniz Aodax, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe.

Dk. Aodax alisema kuwa ili kuondokana na vifo vitokanavyo na uzazi kwa mama na mtoto, wanatumia kliniki hiyo kuwafikia na kuelimishwa wajawazito umuhimu wa kujifungulia kituoni badala ya nyumbani.

Alisema huduma hiyo imesaidia kuongeza idadi ya wajawazito kujifungulia kwenya vituo vya afya ikilinganishwa na awali.

Alisema kila mwezi wanapokea wastani wa wajawazito kuanzia 15 na kuendelea kutoka 10 kwenye vituo hivyo kabla ya kuanza kutoa huduma hiyo.

Alisema baada ya kufuatilia, walibaini wengi wanajifungulia nyumbani kwa kukosa elimu ya umuhimu wa kwenda hospitalini na kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito kutokana na umbali viliko vituo vya afya.

"Vijiji vya Ibanza, Bunonga na Kitongoji cha Witasisa vipo pembezoni mwa kata, hivyo inatulazimu kuvifikia kila mwezi na kuwapatia huduma ya kliniki wajawazito na wakati huo ndio tunaotumia kuwaelimisha sasa wameitika wito tofauti na ilivyokuwa hapo awali," alisema Dk. Aodax.

Alisema tatizo lililopo kwa sasa ni wanafunzi wanapopata mimba wakiwa bado masomoni, wazazi wanawaficha na kushindwa kujitokeza kuanza kliniki mapema ili kujua maendeleo ya mtoto tumboni badala yake wanakwenda wakiwa wana vichanga mkononi.

Ofisa Mendeleo ya Jamii wa Kata hiyo, Sophia Philbert, alisema awali alikuwa akipokea malalamiko ya wajawazito wengi kujifungulia nyumbani bila sababu za msingi na kuhudhuria kliniki wakiwa na wakiwa na vichanga.

Kwa mujibu wa Sophia, kila mwezi anahakikisha huduma hiyo ya kliniki tembezi inawafikia wajawazito wote katika vijiji vilivyopo pembezoni kwa ajili ya kuwapatia elimu ya uzazi salama, ikiwamo kupima Virusi vya Ukimwi (VVU) wakiwa na wenza wao.

Mkazi wa Kijiji cha Bunonga Elizabeth Juma, alisema mtoto wake wa kwanza alijifungulia nyumbani kwa msaada wa jirani yake na hakuwahi kuhudhuria kliniki.

Elizabeth, alisema baada kutembelewa na kuelimishwa amebaini umuhimu wa kwenda kliniki wakati wa ujauzito na kujifungulia hospitalini ili kuokoa maisha yake na mtoto.

## Watumishi waonywa, wanafunzi wasichana watoroshwa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKUU wa Mkoa Wa Mara, Evance Mtambi, ameonya kuwa atawachukulia hatua kali watumishi wasio waadilifu kwa kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mtambi alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akikagua ujenzi wa soko jipya la mji wa Tarime.

" Watumishi wa serikali mliopo hapa nataka mnielewe sitasita kumshughulikia mzembe kazini, mla rushwa, mhujumu fedha za miradi ya maendeleo na ubadhirifu wa mali ya umma," alisema.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa soko hilo, alisema umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na kuwepo kwa madai ya changamoto za upatikanaji kokoto, mvua zinazoendelea kunyesha na malipo kwa mkandarasi zaidi ya Sh. bilioni moja.

Mtambi alisema serikali ilishatoa fedha kwa kukamilisha ujenzi huo na kumtaka mkandarasi kuhakikisha unakidhi viwango vilivyotakiwa na vipimo sahihi bila kuhujumiwa.

"Tarime Vijijini nimepita Kata ya Mriba Tarafa ya Ingwe ninaambiwa kuna utoro wanafunzi zaidi ya 40 wa kike wameshindwa kuhudhuria masomo bila sababu, baadhi yao huenda wametoroshwa. Wazazi, walimu, uongozi wa kata na tarafa wanatakiwa kufuatilia utoro huo ili waliowatorosha wachukuliwe hatua za kisheria," alisema Mtambi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime Mji, Gwimbana Ntovya, alisema ujenzi wa soko hilo umekamilika kwa asilimia 87.

Ntovya, alisema kilichobakia ni kukamilisha sehemu ya mbele na kuweka milango.

" Kuna vibanda 325 vya maduka, vizimba 160, bucha tatu, migahawa miwili, duka la super market na benki mbili," alisema.

Alisema endapo ujenzi wa soko hilo utakamilika Mei 17, mwaka huu utaiwezesha halmashauri hiyo kukusanya mapato ya zaidi ya Sh. milioni 588 kwa mwezi na kutumika kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo na kuboresha huduma za jamii.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UCHUKUZI

## HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI MHE. PROF MAKAME MNYAA MBARAWA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25









MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (Mb)
WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI







MHE.DAVIDI KIHENZILE
NAIBU WAZIRI UCHUKUZI



Prof. Godius Kyarara
KATIBU MKUU UCHUKUZ





DKT. ALLY S. POSSI
NAIBU KATIBU MKUU UCHUKUZI.

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

## A: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka kuwa, tarehe 30 Agosti, 2023 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Wizara ya Uchukuzi baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tangu kuundwa kwake, Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza kazi zake kulingana na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu iliyotolewa. Kwa heshima kubwa, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Uchukuzi. Ninaomba kumhakikishia Mhe. Rais na Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uaminifu mkubwa ilikuliletea Taifa letu maendeleo. Kwa muktadha huo, naomba kutoa Hotuba yangu ya kwanza ya Wizara ya Uchukuzi ambayo imejikita katika masuala ya usimamizi na uwezeshaji wa maendeleo ya miundombinu, huduma za uchukuzi na hali ya hewa kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu kwa Wananchi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi baada ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kugawanywa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, niruhusu nitumie fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka mitatu (3) katika uongozi wake mahiri ulioleta mafanikio makubwa. Pamoja na juhudi nyingine, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za uchukuzi ikiwemo: ujenzi wa reli ya *Standard Gauge Railway* (SGR); uboreshaji wa bandari; ukarabati na ujenzi wa meli; ujenzi wa boti za utafutaji na uokoaji katika Maziwa Makuu; uendelezaji wa viwanja vya ndege; ununuzi wa mitambo ya kuongozea ndege; ununuzi wa ndege; ununuzi wa rada za hali ya hewa; na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika Vyuo vinavyosimamiwa na Wizara.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utendaji na kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo Wananchi na Taifa kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa, utendaji wake umeleta chachu kubwa katika utendaji wa Serikali ya Awamu ya Sita.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa uongozi wake makini. Kwa hakika kazi anazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ndani na nje ya Bunge zimekuwa na ufanisi mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nimpongeze Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo. Kwa hakika Naibu Waziri Mkuu ameonesha umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yake.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa na pia kwa heshima kubwa nakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Tunakuombea M/Mungu aendelee kukupa afya njema ya kutekeleza majukumu yako ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, nimpongeze Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yake katika kumsaidia Spika kuliongoza Bunge. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), kwa kuendelea kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nawapongeza Mheshimiwa **Dkt. Joseph Kizito Mhagama**, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa **Deo Philip Mwanyika**, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuteuliwa kushika nyadhifa za uenyekit wa Bunge. Pia niwapongeze Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) waliokuwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Wizara za: Uchukuzi na Mambo ya Ndani ya Nchi, mtawalia.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb.). Sambamba na viongozi hao wa Kamati, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati. Kamati hii imeendelea kutoa maelekezo na ushauri wenye tija kwa Wizara.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa simanzi kubwa nichukue fursa hii kutoa pole nyingi kwa Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha Hayati Mhe. **Ali Hassan Mwinyi**, aliyekuwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Pili kilichotokea tarehe 29 Februari, 2024 na kifo cha Hayati Mhe. **Edward Ngoyai Lowassa,** aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne kilichotokea tarehe 10 Februari, 2024. Hakika tutaendelea kujifunza kutokana na utumishi wao katika kulitumikia Taifa. Aidha, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Hayati Mhe. **Francis Leonard Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kilichotokea tarehe 1 Julai, 2023 na kifo cha Hayati Mhe. **Ahmed Yahya Abdulwakil** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani kilichotokea tarehe 8 Aprili, 2024. Tutaendelea kuthamini na kuenzi michango yao katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa hali ya utekelezaji wa ujumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka 2023/24 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka 2024/25 katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Uchukuzi.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nitoe taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

## B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

1. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa wa ukuaji wa Uchumi kwa Taifa kwa kuwa ni sekta wezeshi katika kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za uzalishaji zikiwemo sekta za kilimo, madini, utalii, viwanda na biashara. Mathalan, katika mwaka 2022 Sekta ya Uchukuzi ilikua kwa asilimia 3.80 na kuchangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 6.70. Aidha, Sekta hii ni ya tatu 3) kwa kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma (Trade in Services). Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu, mchango wa sekta hii katika fedha za kigeni umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Dola za Marekani bilioni 1.6 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 50 katika kipindi hicho.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 2.089** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 118.215** ni za Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi zake na **Shilingi Trilioni 1.971** ni za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Trilioni 1.827** sawa na asilimia 87.48 ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi Bilioni 71.125** ni fedha Za Matumizi ya Kawaida ambazo ni sawa na asilimia 60.16 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa; na **Shilingi Trilioni 1.756** ni fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 89.12 ya bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Uchukuzi iliendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati.

**Udhibiti wa huduma za Usafiri wa Anga**

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa usafiri wa anga nchini.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024, TCAA ilifanya uchunguzi na kusajili ndege 15 ambazo zilipewa vyeti vya ubora (Certificate of Airworthiness). Aidha, jumla ya ndege mbili (2) ziliondolewa kwenye Daftari la Usajili baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji. Ndege nyingine 91 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora ili kuendelea kutoa huduma nchini. Ukaguzi huo umewezesha daftari la usajili wa ndege kuwa na jumla ya ndege 419.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa soko la usafiri wa anga nchini kwa kuvutia Mashirika ya ndege ya kimataifa kutoa huduma za usafiri wa anga pamoja na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma, Serikali kupitia TCAA imeendelea kusaini mikataba mipya na kuipitia mikataba iliyopo ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) baina ya Tanzania na nchi nyingine. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali ilifanikiwa kusaini Hati za Makubaliano tano (5) za nchi za Poland, Suriname, Algeria, Jamhuri ya Czech na Ivory Coast. Makubaliano hayo yaliyosainiwa yanaifanya Tanzania kuwa na Mikataba ya BASA na nchi 85 ikilinganishwa na nchi 80 iliyokuwa imeingiwa hadi kufikia mwaka wa fedha 2022/23. Mikataba ya BASA imewezesha Mashirika 25 ya ndege za kimataifa kutoa huduma nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika***, TCAA pia iliratibu shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo ambapo hadi kufikia Machi, 2024 abiria waliosafiri kwa kutumia usafiri wa anga wameongezeka hadi abiria 5,080,920 ikilinganishwa na abiria 4,105,375 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022/23, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 23.76. Vilevile, mizigo iliyosafirishwa imeongezeka hadi kufikia tani 27,532 ikilinganishwa na tani 23,070.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 19.33.

*(Utendaji wa utoaji wa huduma za usafiri wa anga na utekelezaji wa miradi kupitia TCAA umeainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia **uk 14 hadi uk 23).***

**Udhibiti wa Usafiri Ardhini**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa Usafiri Ardhini unaojumuisha usafiri kwa njia ya barabara, usafiri wa reli, na usafiri kwa njia ya waya unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni, Serikali kupitia LATRA imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi na vichwa vya treni kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyombo (Vehicle Tracking System – VTS). Hadi kufikia Machi, 2024 mabasi 10,270 yanayotoa huduma ya usafiri wa masafa marefu na vichwa vya treni 20 (TAZARA - 18 na TRC - 2) vimeunganishwa katika mfumo huo. Matumizi ya mfumo huo yamepunguza ajali zitokanazo na mwendokasi na kuongeza ufanisi wa vyombo vinavyodhibitiwa ambapo kwa mwaka 2022/23 ajali zilipungua hadi kufikia ajali 166 za mabasi ya masafa marefu ikilinganishwa na ajali 179 zilizotokea mwaka 2021/22.

12. ***Mheshimiwa Spika***, utakumbuka kuwa, tarehe 28 Juni 2023, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitangaza hapa Bungeni uamuzi wa Serikali wa kuondoa zuio la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa mwaka 1994. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA ilifanya maandalizi na kuanza kutoa ratiba za mabasi kusafiri nyakati za usiku kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2023. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya ratiba za mabasi 798 zimetolewa kwa ajili ya safari za usiku. Ni dhahiri kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeonesha dhamira ya kweli ya kuifungua nchi kiuchumi.

*(Utendaji wa udhibiti wa usafiri ardhini LATRA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu katika **uk. 23 mpaka uk. 31).***

**Udhibiti wa Usafiri Majini**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa huduma za bandari, usafiri wa majini Tanzania Bara na **kutoa** huduma ya biashara ya meli kwa bidhaa mahsusi.

14. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu usimamizi wa watoa huduma zinazodhibitiwa, Serikali kupitia TASAC imeendelea kutoa leseni na vyeti vya usajili kwa watoa huduma waliokidhi vigezo. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya watoa huduma 1,722 walisajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na jumla ya watoa huduma 1,498 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 14.95.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASAC katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 imeendelea kurasimisha bandari bubu za Tanzania Bara. Katika kutekeleza jukumu hilo, bandari bubu 99 zilikaguliwa na kufanyiwa tathmini ya kina na Serikali kupitia TASAC kwa kushirikishana na Mamlaka mbalimbali za Serekali ambapo bandari 45 zilirasimishwa. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa Serikali inaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya bandari ili kuboresha utoaji wa huduma.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu shughuli za utafutaji na uokoaji, Serikali kupitia TASAC imeendelea kuratibu shughuli hizo kupitia Vituo vya Utafutaji na Uokoaji Majini vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza (Maritime Rescue and Coordination Centre – MRCC).

17. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda chini ya uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kikanda wa Kuboresha Mawasiliano na Uchukuzi Katika Ziwa Victoria wenye lengo la kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji katika Ziwa. Hadi kufikia Machi, 2024 ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kikanda cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokoaji katika Ziwa Victoria (Regional Maritime Rescue Coordination Centre - RMRCC) umefikia asilimia 26. Aidha, ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokoaji unaendelea vizuri.

*(Utendaji wa TASAC umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu **kuanzia uk. 32 mpaka uk. 44**).*

**Huduma za Hali ya Hewa**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea na utoaji wa huduma na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. TMA imeendelea kutoa utabiri wa kila siku, wa siku kumi na ule wa muda mrefu pamoja na tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TMA imekamilisha ufungaji wa rada za hali ya hewa katika mikoa ya Kigoma na Mbeya na kufikisha jumla ya rada tano (5) za hali ya hewa nchini. Aidha, utengenezaji wa rada nyingine mbili (2) unaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2024 na zitafungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma.

*(Utendaji wa TMA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia **uk. 44 mpaka uk. 50)***

**Huduma za Bandari**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia na kutoa huduma zote kibandari katika Bandari zote za TAnzania Bara.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 TPA ilihudumia tani milioni 20.72 ya shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani milioni 14.56 katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 42.31. Aidha, kwa upande wa makasha, TPA ilihudumia makasha 805,167 ikilinganishwa na makasha 688,609 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 16.92. Ongezeko hilo la shehena ya mizigo na makasha limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia, TPA imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa bandari nchini pamoja Bandari Kavu. Aidha, TPA imeendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi nje ya nchi; kutafuta masoko; na kufanya ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika bandari nchini.

23. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, TPA imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali ambapo uchimbaji wa kina umefikia mita 15.5 na upanuzi wa lango la kuingia meli ambalo lina una upana wa mita 200. Kwa sasa, Bandari ina uwezo wa kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305. Aidha, upembuzi yakinifu wa kuboresha Gati Na. 8 – 11 na ujenzi wa Gati Na. 12 - 15 bado unaendelea. Vilevile, mkataba wa kuendeleza miundombinu ya kupokelea mafuta (Single Receiving Terminal - SRT) unaohusisha ujenzi wa matenki 15 ya mafuta (tank farms) pamoja na miundombinu yake, yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 420,000 umesainiwa tarehe 26 Februari, 2024 na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa baadhi ya maeneo ya bandari kwa kuingia ubia na Kampuni Binafsi katika kuendeleza na kuendesha shughuli za bandari kuanzia Gati Na. 4 hadi 7. Kwa sasa hatua mbalimbali zikiwemo za makabidhiano na *mobilization* zinaendelea ili kuruhusu utekelezaji rasmi kuanza. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mwekezaji mwingine atakayekuwa na jukumu la kufanya shughuli za uendeshaji kuanzia Gati Namba 8 hadi 11. Lengo ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari.

*(Utendaji wa TPA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **yangu kuanzia uk. 51 hadi 59)**.*

**Huduma za Usafiri wa Reli Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli iliyopo ya *Meter Gauge*

*Railway* (MGR) yenye urefu wa kilomita 2,706 na kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia reli hiyo. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge Railway* (SGR) ya ushoroba wa kati kwa awamu zote mbili ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilomita 1,219 na awamu ya pili ina jumla ya kilometa 1,590 na hivyo kufanya reli mpya ya SGR inayojengwa kuwa na mtandao wenye jumla ya kilomita 2,809 ambazo ni zaidi ya kilomita 103 ikilinganishwa na reli ya MGR ambayo ilijengwa wakati wa Mkoloni. Pamoja na hatua hiyo, Serikali itaendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo mengine ya Ushoroba wa Kusini na wa Kaskazini kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali iliahidi kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa awamu zote mbili. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Machi 2024, ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 98.93; kipande cha kutoka Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 96.61; kipande cha kutoka Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 56.21; kipande cha Makutupora - Tabora (368 km) umefikia 14.22%, na Tabora - Isaka (165km) umefikia 5.72%. Kwa upande wa awamu ya pili, kipande cha kutoka Tabora – Kigoma (Km 506) umefikia asilimia 1.81; na ujenzi wa kipande cha Uvinza – Musongati – Gitega (km 282) umeanza ambapo hatua za ununuzi wa Mshauri Elekezi na Mkandarasi zinaendelea.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuanza uendeshaji wa treni katika reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia TRC inaendelea na majaribio ya miundombinu ya reli kwa ajili ya kuanza utoaji wa huduma hiyo rasmi ifikapo mwezi Julai, 2024. Aidha, majaribio haya yanafanyika kwa lengo la kukidhi takwa la usalama kabla ya kuanza uendeshaji.

*(Utendaji wa TRC umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu **Ukurasa kuanzia 60 hadi uk.76**).*

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) inamilikiwa na Serikali mbili za Tanzania na Zambia kwa hisa za asilimia 50 kwa 50. Katika kuendeleza huduma za reli kati ya nchi hizo mbili, TAZARA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo, kulinda na kuimarisha miundombinu ya reli yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,153, na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli.

30. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2024, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani za mizigo 251,264 ikilinganishwa na tani 235,071 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 6.89. Ongezeko hilo limechangiwa na ushirikishaji wa sekta binafsi ya Kampuni Ms Calabash Freight Limited na Ms African Inland Container Depot (AFICD). Utaratibu huu umeingizia TAZARA mapato ya Shilingi bilioni 8.91 kutokana na Kampuni hizo kulipia tozo.

31. ***Mheshimiwa Spika***, treni za abiria zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi na ile inayosafiri kati ya stesheni za Kidatu na Makambako zilisafirisha jumla ya abiria 672,006. Aidha, Treni ya Jijini Dar es Salaam inayofanya safari zake kati ya Stesheni ya TAZARA hadi Stesheni ya Mwakanga - Pugu jijini Dar es Salaam ilisafirisha abiria 1,582,833 ikilinganishwa na abiria 1,447,738 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 9.33. *(Utendaji wa TAZARA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia **uk 76 hadi uk.80).***

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa Makuu**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 MSCL ilisafirisha abiria 198,080 ikilinganishwa na abiria 170,137 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 16.42. Kwa upande wa mizigo, MSCL ilisafirisha tani 33,288.44 ikilinganishwa na tani 18,909 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 76.05. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa ukarabati na kuanza kazi kwa meli ya MV. Umoja ambayo ilianza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2023 katika Ziwa Victoria kati ya Bandari ya Mwanza Kusini na Bandari za Port bell na Jinja, Uganda.

35. ***Mheshimiwa Spika*** Aidha, ujenzi wa Meli ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu umekamilika kwa asilimia 95 na tayari meli hiyo imefanyiwa majaribio ziwani ya mifumo na mitambo.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia MSCL ilisaini Mkataba wa ujenzi wa meli mpya ya kubeba mizigo ya tani 3,000 katika Ziwa Victoria. Pia ilisaini mikataba 2 ya ujenzi wa meli ya mizigo ya tani 3500; na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi wa kiwanda hiki ni hatua muhimu ya kujivunia kwa Taifa letu kwa kuwa ni mara ya kwanza kujenga kiwanda cha aina hii hapa nchini ambapo kwa miaka ya nyuma meli nyingi zilikuwa zinatengenezwa nje ya nchi. Vilevile mradi wa ukarabati wa Mv. **Liemba tayari umesainiwa.**

*(Utendaji wa MSCL umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia **uk.81 hadi 86**).*

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ina jukumu la kuendesha na kuendeleza Viwanja vya Ndege 58 vya Serikali vilivyopo Tanzania Bara. Hadi kufikia Machi 2024, TAA ilihudumia jumla ya abiria 3,202,573 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.58 ikilinganishwa na abiria 2,949,508 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa, hadi kufikia Machi 2024, TAA ilikamilisha ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilometa 7.2 na ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma. Aidha, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ufungaji wa mfumo wakamera za usalama (CCTV) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika kwa asilimia 100.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuwa na viwanja vya ndege vyenye ubora, TAA imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo ujenzi wa jengo jipya la abiria umekamilika kwa asilimia 98. Majengo mapya ya abiria katika viwanja vya ndege vya Kahama na Kilwa Masoko; yamekamilika wakati ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mpanda umekamilika kwa asilimia 97. Aidha, Usanifu wa Kina wa Jengo la Mnara wa Kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba umekamilika na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi zinaendelea.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jukumu la ujenzi wa viwanja vya ndege litarijeshwa rasmi TAA kwa utaratibu maalum ambao hutoathiri miradi iliyokuwa imeanza kutekelezwa na TANROADS. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa jukumu hilo sasa limerejeshwa na linatekelezwa na TAA kwa miradi mipya na miradi iliyo chini ya asilimia 40 ya utekelezaji. Baada ya uamuzi huo, TAA imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Moshi, Lindi, Mtwara, Mwanza na JNIA (Jengo la Pili la Abiria – TB II).

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kukuza fursa za ajira na uhaulishaji wa teknolojia (technological transfer) kwa wazawa, Serikali kupitia TAA imewezesha uwekezaji wa kiwanda cha uunganishaji na utengenezaji wa ndege ndogo katika Kiwanja cha Ndege cha Morogoro kupitia Kampuni ya *Airplane Africa Limited*. Kampuni hiyo inafanya kazi ya kuunganisha na kutengeneza ndege za kubeba abiria wawili (2) ambazo ni aina ya "Skyleader". Kwa sasa kiwanda hicho ni cha pekee Afrika Mashariki ambapo kina matawi katika nchi za Urusi, Jamhuri ya Czech, Ujerumani na China.

**Huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA)**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2023/24 niliahidi kuwa Serikali inaendelea na taratibu za kurejesha shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kutoka KADCO. Napenda kulitaarifu rasmi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha urejeshwaji wa Kiwanja cha KIA kwa TAA kutoka KADCO,na kiwanja hicho kwa sasa kinaendeshwa na TAA.

*(Utendaji wa TAA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia **uk 86 hadi 98**).*

**Huduma za Usafiri wa Anga**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha utendaji wa Shirika la Ndege, Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya na kuboresha miundombinu wezeshi ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo na karakana. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali ilikamilisha malipo ya ndege tatu (3): ndege 2 za Boeing 737- 9 Max tayari zilishawasili nchini na zinafanya kazi na 1 ya Boeing 787-8 Dreamliner itawawasili mwishoni mwa mwezi huu. Kuwasili kwa ndege hizi kutaifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 16.

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuongeza wigo wa huduma zake, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 24 ambapo vituo 13 ni vyandani na vituo 11 ni vya nje ya nchi. Vituo vya ndani ya nchi ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kilimanjaro,





Kigoma, Songwe, Mpanda, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar. Vituo vya nje ya nchi ni Bujumbura, Dubai, Entebbe, Hahaya, Guangzhou, Harare, Lubumbashi, Lusaka, Mumbai, Nairobi na Ndola.

46. ***Mheshimiwa Spika***, uboreshaji wa ATCL umeongeza utendaji wa ATCL ambapo hadi kufikia Machi, 2024, ATCL ilisafirisha abiria 850,660 ikilinganishwa na abiria 826,594 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 2.91. Vilevile**,** ATCL iliweza kusafirisha jumla ya tani 5,034.2 za mizigo ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 2,680.9 katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimi 87.78. Ongezeko hilo limetokana na kuanza kufanya kazi kwa ndege ya mizigo aina ya Boeing 767-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54.

***(****Utendaji wa ATCL umeainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia* ***uk.98 hadi uk. 107)***

**B. 1: VYUO VYA MAFUNZO YA KISEKTA**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uwezo na kutumia wataalam wa ndani pamoja na kupunguza gharama za kusomesha wataalam nje ya nchi. Serikali kupitia vyuo vya kisekta vinavyosimamiwa na Wizara ya Uchukuzi, imeendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za mafunzo ya usafiri wa anga, usafiri ardhini na usafiri majini kwa lengo la kuzalisha wataalam wanaotoa huduma katika Sekta ya Uchukuzi.

*(Utendaji wa Vyuo vya Mafunzo vya Kisekta umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia* ***uk.107 hadi uk. 122)***

**B. 2: MAFANIKIO YA MIAKA MITATU (3) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba miradi ya maendeleo ya sekta ya uchukuzi ni miongoni mwa miradi ambayo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutekelezwa bila kusuasua na kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi hicho, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati inayojumuisha: miradi ya reli; viwanja vya ndege; uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania; ujenzi na uboreshaji wa bandari; ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; ufungaji wa rada za hali ya hewa; na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muhtasari yapo mafanikio mengi na makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi kifupi cha miaka mitatu ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Mafanikio hayo ni pamoja na: kuongeza wigo wa Reli ya SGR kwa kuifanya kuwa ya kikanda ambapo Serikali hii imeweza kuanza mikakati ya kuifikisha reli ya SGR nje ya mipaka ya nchi; kuendelea kuboresha kwa kasi huduma za meli, ambapo baadhi ya meli zimeanza kujengwa na kukarabatiwa; kutekeleza kwa vitendo mipango ya uboreshaji wa bandari nchini kwa Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kushirikisha sekta binafsi; kuanzishwa kwa Mafunzo ya urubani nchini kwa mara ya kwanza tangu kupata uhuru; na kubuni na kutekeleza mikakati iliyoondoa foleni ya Malori katika Mpaka wa Tunduma. *(Mafanikio yalipoatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita yakiwemo ya mwaka wa fecha wa 2023/24 yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia* ***uk. 132 hadi 146).***

**B. 3: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUZITATUA**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua imeoneshwa katika *Kitabu cha Hotuba yangu* ***uk. 147 hadi uk. 150).***

**C: MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2024/25, husuan bajeti ya miradi ya maendeleo ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati inayoendelea.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,729,676,417,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 114,744,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,614,931,941,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 86,661,930,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 28,082,546,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 2,524,369,202,000 ni** fedha za ndani na **Shilingi 90,562,739,000 ni** fedha za nje.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya ukrabati na Ujenzi wa Viwanja vya ndege nchini, Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria; Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP); Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR; Mradi wa Ukarabati wa Reli ya MGR; Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga; Mradi wa Ukarabati wa Reli ya TAZARA; Mradi wa Ununuzi wa vifaa na Miundombinu ya Hali ya Hewa; Mradi wa uboresheji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu ikiwemo Mv Liemba na Mv Muongozo; Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Mawasiliano ya Ndege (VHF Navigation Aids); Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia katika Vyuo vya DMI na NIT;

*(Maelezo ya kina na kazi zitakazofanyika katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa kila mradi wa maendeleo na fedha zilizotengwa yameainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia* ***uk.153 hadi uk. 173****).*

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa na Wizara kupitia Mapato ya Ndani ya Taasisi zilizo chini yake zimeanishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu **uk.173 hadi uk. 209.**

**D: SHUKRANI**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24. Ufanisi huo ulipatikana kutokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kuishauri Serikali ipasavyo katika masuala mbalimbali husussan yanayogusa maendeleo ya wananchi moja kwa moja. Pia, niwaombe wananchi na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kuijenga na kuikarabati.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kutambua mchango unaotolewa na viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara, nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa **David Mwakiposa Kihenzile** (Mb.)**;** Katibu Mkuu, **Prof. Godius Walter Kahyarara** na Naibu Katibu Mkuu **Dkt. Ally Saleh Possi**. Pia, kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Wizara kutoa shukrani zetu za dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara wamechangia katika utekelezaji majukumu ya Wizara. Kwa namna ya kipekee niruhusu niwatambue wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO); Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini (IMO); Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Japan (JICA); Korea Kusini (KOICA); Ujerumani (KfW); Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Trade Mark Africa; Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki – EAC; Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC; Nchi za Urusi; Umoja wa Falme za Kiarabu-UAE; Uingereza; Marekani; Uholanzi; Japan; India; China; Denmark orea Kusini; Ufaransa; Ubelgiji; Ujerumani na Uturuki; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF; Taasisi za fedha za CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC na TCB na Asasi mbalimbali za kiraia; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sikuwataja hapa kutokana na uwingi wao.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee niruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na kwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**E: MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,729,676,417,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 114,744,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,614,931,941,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

64. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuhusu kazi zinazotekelezwa na Wizara. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hotuba hii. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.uchukuzi.go.tz**).

65. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.





# Operesheni ondoa mifugo bado kizungumkuti Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

LICHA ya kuwapo kwa operesheni za kuondoa mifugo ndani ya Bonde la Ihefu lililopo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, imebainika bado kuna makundi mengi hali inayotishia kupotea kwa ikolojia ya hifadhi hiyo na kukithiri kwa migogoro.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Jenerali Mstaafu, George Waitara aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa ofisi ya shirika hilo Kanda ya Kusini iliyojengwa katika Kata ya Rujewa wilayani hapa Mkoa wa Mbeya.

Waitara, alisema alibaini uwepo wa mifugo hiyo alipokuwa kwenye ndege akielekea kwenye uzinduzi wa ofisi hiyo.

Aliwataka watendaji wa TANAPA kushirikiana na viongozi wa Mbarali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuheshimu mipaka.

Alisema uwepo wa mifugo hiyo ndani ya hifadhi kunasababisha migogoro ambayo haina sababu na kuwataka wafugaji kuiondoa ili kuepuka migogoro hiyo.

Waitara, alisema hifadhi hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na viumbe wengine kutokana na kubeba uhai wa Mto Ruaha Mkuu ambao maji yake yanatumika kwa umwagiliaji, uzalishaji umeme kwenye mabwawa ya Mtera, Mwalimu Nyerere na matumizi mengine.

“Nikiwa angani nimeona bado kule hifadhini kuna mifugo mingi, sasa naomba tuendelee kutoa elimu na kuwahamasisha waondoe mifugo, ikolojia ya hifadhi hii ni muhimu sana kwa maisha yetu kwa hiyo lazima tushirikiane kuilinda,” alisema.

Alisema endapo hifadhi hiyo itaharibika, usalama wa mifugo inayoingizwa itakuwa hatarini kwa kuwa ustawi wake unategemea maji ya mto huo.

Diwani wa Kata ya Mapogoro, Paul Kittah, alisema baadhi ya wananchi hawana uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya uhifadhi na kuwashauri watendaji wa TANAPA kuendelea kutoa elimu.

Kittah, aliwaomba maofisa wa shirika hilo kutotumia nguvu kupita kiasi wakati wa kushughulikia migogoro hiyo na wananchi ili kuepuka uchochezi.

Alisema katika baadhi ya maeneo wananchi wanaingia hifadhini kutokana na kutofahamu mipaka, hivyo akaomba elimu itolewe ya kutosha hasa kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi.

Kamanda wa Uhifadhi Kanda ya Kusini, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Steria Ndaga, alisema wamekuwa wakishirikiana na wananchi kwenye mambo mbalimbali ikiwamo uchangiaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema wamekuwa wakichangia ujenzi wa shule, zahanati, vituo vya afya na madawati kwenye shule ambazo zipo vijiji vya jirani na hifadhi.

Hivi karibuni TANAPA ilitangaza kupiga mnada zaidi ya mifugo 500 ambayo ilikamatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, lakini bado tatizo hilo linaendelea.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, akiwaonyesha waandishi wa habari (hawapo pichani), jana misokoto ya bangi ambayo imekamatwa katika operesheni iliyofanywa na Jeshi la Polisi. Alisema katika kipindi cha kuanzia Februari hadi Aprili mwaka huu watuhumiwa 235 wa makosa mbalimbali walikamatwa. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mradi wasaidia watoto 7,000 Mbeya

**Na Faustine Feliciane**

WATOTO zaidi ya 7,000 kutoka vijiji 37 wilayani Rungwe mkoani Mbeya wanaoishi katika mazingira magumu wamepewa msaada wa malazi, afya na elimu na Shirika la Africa Bridge.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Barry Childs aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kitabu alichokiandika cha kuwajenga watoto na kuwapa maarifa kwenye kilimo na kuwaondoa kwenye umaskini kiitwacho ‘And the Children shall Lead Us’,

Childs alisema alirudi Tanzania baada ya miaka 35 na kuumizwa na hali aliyoikuta kwa watu maeneo ya vijijini na kuamua kuanzisha shirika hilo la kutoa msaada.

Alisema mpaka sasa amewasaidia watoto zaidi ya 7,000 mkoani humo na kuwawezesha kwenda shule, kuwa na sehemu nzuri za kuishi na kugharamia masuala ya afya.

Alisema muundo unaotumiwa na shirika hilo ni kushirikisha watoto wenyewe na wazazi na pia kushirikisha jamii husika kupiti kamati za vijiji ili kuwasaidia katika malezi ya watoto kuanzia shule, nyumbani na kwenye jamii.

Alisema kupitia mradi huo, watoto wanajifunza ujasiriamali kama kufuga ng’ombe, kukamua maziwa, kuuza na upandaji zao la parachichi kwa ajili ya biashara.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo kutoka Wilaya ya Rungwe, Sarah Mosses (22) ambaye kwa sasa anasoma Chuo cha Rungemba Mafinga, alisema mradi huo umemsaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo yake.

## Njombe yavuka lengo chanjo saratani ya kizazi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe mkoani hapa imevuka lengo kwa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wenye umri kati ya miaka tisa hadi 14 kitaifa kwa asilimia 80.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa Chanjo wa Halmashauri ya Mji huo, Simon Ngassa wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki iliyopita.

Ngassa alisema licha ya changamoto walizopitia, lakini wamefanikiwa kutoa chanjo kwa wasichana hao kwa asilimia 91 shuleni na mikutano ya hadhara baada ya elimu kutolewa.

Alisema wasichana ambao bado hawajafikisha umri, wataendelea kupata chanjo kwenye utaratibu wa kawaida na kwamba matarajio ifikapo Desemba mwaka huu nao wataingia kukamilisha asilimia ambazo zimebaki.

Alisema halmashauri hiyo bado ina chanjo za kutosha na kutoa wito kwa wasichana kuendelea kufika kwenye vituo vya afya kupata huduma hiyo.

Mmoja wa wakazi mjini Njombe, Laulian Sanga, alisema wanashukuru wahudumu wa afya kwa kutoa elimu juu ya chanjo hiyo ili kuwakinga wasichana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema elimu zaidi inapaswa kutolewa ili wasichana waweze kuwa salama na jamii kuacha na dhana potofu kuwa chanjo hiyo ina madhara kwa binadamu.

## Chunya yajitosa migogoro ya wakulima, wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya mkoani Mbeya imeanza kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kuanzisha kongani za malisho ya mifugo.

Lengo likiwa ni kupunguza mwingiliano wa mifugo na kilimo na shughuli zingine za uzalishaji.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mbarak Batenga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye mkutano wa robo ya tatu wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo.

Batenga, alisema halmashauri hiyo imekamilisha hatua za awali za kuainisha maeneo ambayo yatakuwa na kongani hizo.

Batenga alisema mpango huo utakuwa shirikishi kwa wananchi wa maeneo hayo na kuagiza viongozi wa kata na vijiji kujadili namna ya kupeleka wazo hilo kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Bosco Mwanginde, aliwataka madiwani kushirikiana na wataalamu kusimamia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao ili ikamilike kwa wakati.

Diwani wa Kata ya Lualaje, Tusalimu Mwaijande, aliahidi kwenda kuwaelimisha viongozi wa kata na vijiji katika maeneo ambayo kongani za malisho zitawekwa.



# Viongozi wa dini watakiwa kutumia matokeo Sensa ya Watu na Makazi

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini wametakiwa kuyatumia na kuyasambaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi kwa sababu wanauwezo wa kufikisha taarifa kwa jamii, hali itakayosaidia serikali kupanga mipango kulingana na takwimu zilizopo.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Muhammad Haji Hamza, aliyasema jana wakati akifungua uwasilishaji wa matokeo ya sensa kwa viongozi wa dini.

Alisema viongozi wa dini ni muhimu kuyajua na kuyatumia matokeo hayo katika huduma za kiibada ikiwamo masuala ya ndoa na talaka.

Alisema katika kuanza mchakato wa sensa viongozi wa dini walitoa mchango mkubwa katika kufanikisha zoezi hilo kwa kutoa elimu katika maeneo yao ya ibada na mafundisho ya dini hivyo ni vyema wakajua matokeo hayo.

Alisema taasisi za dini ni miongoni mwa taasisi ambazo zinahusika katika kutoa elimu, hivyo taarifa hizo zitasaidia kwa kujua uhitaji unaotakiwa katika maeneo kulingana na idadi ya watu waliopo katika maeneo husika.

Akiwasilisha matokeo ya sensa kuhusu masuala ya ndoa, talaka, vizazi na vifo Zanzibar, Mratibu wa Sensa, Abdulmajid Jecha aliwataka viongozi wa dini kuwashawishi jamii kusajili na kutoa taarifa zao kwa maendeleo ya nchi.

Alisema kufanya hivyo itasaidia serikali kupata takwimu halisi za matukio hayo yanayotokea katika jamii na kufanyiwa kazi kwa mujibu wa uhalisia.

Alisema bado kuna changamoto kubwa katika kupata taarifa halisi hasa za ndoa, takala na vifo kutokana na jamii kutoona umuhimu wa kusajili matukio hayo.

Alisema kwa mwaka 2023 vizazi vilivyosajiliwa ni 43,943, kwa Mkoa wa Mjini ni 6,905, Mkoa wa Kusini ni 1582.

Aidha, akitaja takwimu za vifo kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ni 2,859 sawa na asilimia 59 na Mkoa wa Kusini Unguja ni 72.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Salum Kassim Ali, alisema elimu zaidi inahitajika kwa jamii katika suala la usajili wa matukio ya kijamii na lengo la kusajili matukio yote ni kutoa taarifa na takwimu za matukio hayo kila muda ili kufanyiwa kazi.





Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah, akisukuma mkokoteni wakati akifanya usafi na wananchi katika soko kuu la Muheza na stendi ya mabasi ya kwenda Bombani jana, pia aliwasihi wananchi umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mama Mwinyi 'awafunda' wakunga utoaji huduma bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Maryam Mwinyi, amewataka wakunga kuwa na upendo, huruma na kufuata maadili ya taaluma zao pamoja na kutoa huduma bora kwa wajawazito.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani iliyofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema serikali imeweka mikakati ya kuimarisha afya ya uzazi ili kupunguza vifo vya mama na watoto wachanga vitokanavyo na uzazi.

Mama Maryam ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Maisha Bora Foundation, alisema wakunga wenye tabia ya kuwanyanyasa wagonjwa wanapaswa wachukuliwe hatua za kisheria.

Alisema wakunga wanamchango mkubwa katika kufanikisha malengo yaliopangwa na serikali sambamba na kuiomba jamii kuwatumia wakunga hao ili kuepuka matatizo yanayoepukika.

Aidha, alisema katika kuhakikisha huduma hizo zinazidi kuimarika Rais Hussein Ali Mwinyi alimteua Mkurugenzi wa Uuguzi na Ukunga kwa lengo la kuweka usimamizi na kuleta mabadiliko katika kutoa huduma bora kwa wagonjwa hasa mama na mtoto.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema wizara inaimarisha vituo vya afya ya msingi ili kumaliza tatizo la mama na mtoto na wizara ina mpango wa kuongeza watendaji katika maeneo yote ili kupunguza changamoto ya upungufu uliopo katika maeneo hayo.

Aidha, alisema wizara itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwatumia wafanyakazi wa afya ngazi ya jamii na kuwapa elimu ya lishe ili kuimarisha huduma za mama na mtoto pamoja na kuwapatia mafunzo ya msingi ya dharura kwa wajawazito.

Akizungumza kwa niaba ya Jumuiya ya Wakunga, Sanura Abdalla Salim, alisema lengo la kuanzishwa kwa jumuiya hiyo ni kuisaidia serikali kuimarisha huduma za afya hasa ya mama na mtoto.

Alisema wamejipanga kuimarisha utoaji wa huduma bora ili kuendeleza heshima ya wakunga na kutetea haki za wajawazito ikiwamo kupatiwa huduma zenye heshima za uzazi katika jamii na kwenye vituo vya afya.

Aidha, alisema wakunga wanakabiliwa na changamoto ikiwamo ufinyu wa elimu ya utambuzi, upungufu wa vitendea kazi kama vifaa vya kisasa vya kusikiliza mtoto tumboni, uhaba wa wakunga na wauguzi katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma.

## Shule za msingi, sekondari kuunganishwa na TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Leila Muhammed Mussa, amesema serikali imewekeza katika mifumo ya Tehama, ili wanafunzi na walimu wasiwe nje ya dunia katika masuala ya teknolojia.

Aliyasema hayo juzi wizarani kwake Mazizini wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya miaka mitatu ya maongezi ya awali kati ya Wizara ya Elimu na kampuni ya Enkisoma Afrika kutoka Kenya inayojishughulisha na masuala ya Tehama katika elimu.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha upo mradi mkubwa unaolenga kuziunganisha shule zote mpya na kongwe katika mkonga wa taifa, ili kuwasaidia walimu kufundishia.

Alisema pia serikali kupitia Wizara ya Elimu imenunua kompyuta mpya zaidi ya 1,500 kwa ajili ya wanafunzi pamoja na vishikwambi kwa walimu kufundishia.

Leila alisema makubaliano hayo na kampuni hiyo yatahusisha kuwajengea uwezo walimu jinsi ya kuvitumia vifaa hivyo mashuleni ili yatapokamilika wawepo wataalamu wa kutosha wa kuvisimamia vifaa hivyo.

Alisema kampuni hiyo pia itakuwa inasambaza vifaa vya Tehama mashuleni ili kupunguza changamoto ya miundombinu ya Tehama katika shule za Zanzibar.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Enkisoma Afrika, Sankei Ole Kenga, alisema kwa sasa dunia imebadilika, hivyo mambo ya teknolojia ni muhimu katika kufanya kazi mbalimbali hususani kwa wanafunzi.

Alisema iwapo wanafunzi wakajifunza mambo ya teknolojia itawasaidia kuwawezesha kufanya vizuri katika masomo yao na kupata mbinu ya kujiajiri na watasimamia vizuri mifumo hiyo ili lengo la makubaliano hayo kufikiwa.

Mkurugenzi Idara ya Tehama kutoka Wizara ya Elimu Zanzibar, Mbwana Yahya Mwinyi, alisema kwa sasa shule tisa mpya tayari zimeunganishwa na mkonga wa taifa, ili kupunguza changamoto ya intaneti.



Alisema mkakati wa serikali ni kuziunganisha shule zote za Zanzibar katika mkonga huo ili walimu na wanafunzi waendane na malengo ya kidunia.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**WILSON GEORGE WILSON** naomba kutangaza kupotelewa na hati ya kusafiria Namba **TAE517973** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mwaka 05/10/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/80479/2024.**

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SHANI SAID MAYOSA** naomba kutangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TSE010993** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mwaka 22/03/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/38520/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SELEMANI IDDI BAKARI,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 783 BZL**. Chassis no **Id3pck6jxj2003622.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI:. **PHQ/DOD/DOD/16075/2024.**

### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FEDRICK ANDREA NYALUKE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI **MC 608** BUY. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE. POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/5548/2024.**

### KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**AMANI DANFORD MLAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 427 CWK** aina ya **DAF.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/79170/2024.**

### KUPOTEA KWA OFFER YA KIWANJA

Ndugu **ELIUD NYAUHENGA** anatangaza kupotelewa na offer ya kiwanja yenye jina **HUSSEIN HARIRI** mmiliki wa awali **Plot No. 136, Block C, Ilozo South** iliyotolewa na Mamlaka ya ustawishaji Makao Makuu Dodoma tarehe 03/11/2004. Kwa sasa kiwanja kinamilikiwa na **ELIUD T. NYAUHENGA.** Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/16618/2024.**

### KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**JAMAL ANDREA NKWERA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 781 DQZ** aina ya **TOYOTA RACTIS.** Chassis namba **NCP10000506677.** Engine namba **NCP10577.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/80257/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU**

**MASIJALA NDOGO YA GEITA**
**GEITA**

**RUFAA YA ARDHI NO. 8491 YA MWAKA 2024**
**(imetokana na Maombi Namba 24/2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya – Geita)**

**GRACE LAURENT MAPEMBE (Msimamizi wa Mirathi)................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**BONIFACE REUBEN KATAMPA**
**ABDALLAH SHILLAZI ALLY............WAJIBU RUFAA**

**KWA: ABDALLAH SHILLAZI ALLY – POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 21/5/2024 saa mbili na nusu Asubuhi kuja kusikiliza rufaa iliyofunguliwa dhidi yako.
Unatahadharishwa kuwa endapo hautafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu pamoja na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30/04/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU - GEITA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA TALAKA NO 13/2024**

**HENRY MKALANGA....................................MDAI**

**DHIDI**

**ROIDA KACHOTA....................................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Mdaiwa **ROIDA KACHOTA** popote pale ulipo unatakiwa kufika mahakamani
Tarehe 24/05/2024 saa 2:30 Asubuhi kwa ajili ya shauri la Talaka.

Usipofika Tarehe husika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakam hii Leo Tarehe 06/05/2024.

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.7519 OF 2024**

**In the Matter of the Etate of the late UPENDO JEREMIA MSIGWA**

**By 1.MUSSA KITUNGURU ZONZO**
**2.............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 08thd day of MAY2024.
Dated at Morogoro this 29th day of APRIL 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...21/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAMADHANI JUMANNE wa KILAKALA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ELIWAJA JACOB**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 2 Mwezi 6 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 2 mwezi 5 mwaka 2024

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MAOMBI MADOGO NA. 3247 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**KHADIJA SALUM ALI**

**ABUBAKARI ALI ABRAHAM & SULEIMAN YUSUPH...........MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 Mwezi Juni, 2024. Saa 9:30 Asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji G.N. BARTHY.
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 29 Mwezi wa Aprili, 2024.

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...12/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ESTER M. KUGURU WA MOROGORO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KHERI ABDUL MLELWA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 8 Mwezi 5 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 05 mwaka 2024

---

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 8142/2024**

**In the matter of the Estate of the late JONATHAN PETRO MAGAWA of Mwegamile Chihikwi within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAGRETH P. MAGAWA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 06th Day of MAY, 2024

Dated at Dodoma this 16th Day of APRIL, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA

---

**IN THE HIGH COURT TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 165 OF 2018**

**BANK OF BARODA LIMITED................. DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**RAYMOND FOCUS MLAY**
**(Trading as Bumbuli General Supply)............1st JUDGMENT DEBTOR**

**MWANAISHA SALUMU OMARY**
**(Trading as Bumbuli General Supply).........2nd JUDGMENT DEBTOR**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO: RAYMOND FOCUS MLAY T/A BUMBULI GENERAL SUPPLY,**
**P.O. Box 33700, DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTICE** that the decree holder has instituted an application against you with particulars set out in the Application for execution of decree filed in this court, Service of the summons on you has been ordered by means of this publication.
You are directed to collet copies of the summons and application for execution for decree from the court's registry, P.O. Box 12533, Dar es salaam. You are hereby summoned to show cause in this court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 8th day of May, 2024 at 14:00 pm when this case will be heard.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** should you default to enter appearance as herein provided, the application will proceed and a decision may be given in your absence.
Given under my hand and the seal of the Court this 6th day of May, 2024.

DEPUTY REGISTRAR
COMMERCIAL DIVISION
DAR ES SALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA TALAKA NO 13/2024**

**MDAI.........................................BRAC FINANCE LTD**

**MDAIWA.............................................SUZAN MUSA**

**KWA:SUZAN MUSA**

**Shauri la Madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama hii na BRAC FINANCE**

LTD madai ya fedha kiasi cha 1,667,200/=, mdaiwa popote ulipo unaamuriwa kufika kuhudhuria Mahakamani tarehe 15/05/2024 Saa 2:30 Asubuhi kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako kwajili ya kujitetea bila kukosa .Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo Tarehe 30/04/2024.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 7135/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late OMARY ESAU MLULA of Mtumba Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LUCY JACKSON JORAM**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 08 Day of 5, 2024

Date at Dodoma this 9 Day of 4, 2024.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 7134/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late DASTAN SABELI MWIKOLA of Nkuhungu Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SABEL JAPHET WAGILI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 08 Day of 5, 2024
Date at Dodoma this 9 Day of 4, 2024.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 6595/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late GEOFREY SULEIMAN MKAMILO of Area C Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PRISCA GEOFREY MKAMILO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 08 Day of 5, 2024
Date at Dodoma this 9 Day of 4, 2024.

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

ATHARI ZA MAFURIKO KENYA

# Watu waliofariki sasa wafikia 228

- Shule zafungwa kwa muda usiojulikana

Na Maulid Mmbaga

WIZARA ya Mambo ya Ndani nchini Kenya imebainisha kwamba idadi ya watu waliofariki kutokana na mafuriko na athari nyingine za mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini Kenya imeongezeka hadi 237.

Mafuriko hayo yameharibu nyumba, barabara, madaraja na miundombinu mingine katika eneo kubwa la uchumi wa nchi hiyo, ikibainishwa kuwa takriban watu 164 wamejeruhiwa na hali mbaya ya hewa, wakati 212,630 wamelazimika kuyahama makazi yao.

Pia inabainishwa kuwa kutokana na hali mbaya ya hewa nchini Kenya watu 72 wameripotiwa kupotea, huku makazi zaidi ya 42,526 yakiharibiwa, na kwamba shule 1,967 zimeathiriwa na mafuriko, hali iliyosababisha Rais Wiliam Ruto kutangaza shule hizo kufungwa kwa muda usiojulikana.

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo, mafuriko zaidi yanatarajiwa katika maeneo ya tambarare, pembezoni na mijini wakati maporomoko ya udongo/matope yanaweza kutokea katika maeneo yenye miteremko mikali na miinuko.

Aidha, ilielezwa kuwa Rais Ruto aliotoa agizo la kubomolewa kwa nyumba zote ambazo ziko pembezoni mwa mito kama hatua za makusudi za kuwaondoa wananchi katika maeneo hatarishi kwa lengo la kuzuia maafa zaidi kuwakumba.

Mkurugenzi wa Huduma za Hali ya Hewa, David Gikungu, alisema licha ya kudhoofika kwa kimbunga Hidaya, mvua bado inatarajiwa kunyesha katika maeneo ya pwani ya Kenya.

Gikungu alisema kaunti za Kwale, Mombasa, Kilifi na Lamu huenda zikakumbwa na mvua za wastani hadi nyingi.

"Kufuatia kutua kwa kimbunga hicho katika kisiwa cha Mafia Mei 4, mwaka huu, kimbunga Hidaya kilipoteza nguvu kabisa, mabaki ya mawingu ya mvua yaliyoambatana na kimbunga hicho yameonekana kupungua na kusambaa katika maeneo mbalimbali ya ukanda wa kusini mwa Tanzania, kama ilivyothibitishwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania," Gikungu alisema.

Alisema mvua hiyo ya wastani hadi kubwa huenda ikaendelea kunyesha ikiambatana na upepo mkali, huku mawimbi makubwa ya bahari yakiweza kupanda urefu wa mita mbili.

Gikungu alisema maeneo mengine ya nchi pia yanapaswa kutarajia mvua za wastani za mara kwa mara kati ya milimita tano hadi 20 hadi mvua kubwa za kati ya 20-50mm.

**WAKWAMA MBUGANI**

Katika hatua nyingine, ilibainishwa kuwa hali mbaya ya hewa ilisababisha pia watalii kuhamishwa kutoka mbuga maarufu ya Maasai Mara nchini Kenya baada ya mafuriko kukumba sehemu kubwa ya mbuga hiyo.

Mkuu wa polisi wa eneo hilo, Kipkoech Lotiatia, alisema hifadhi hiyo iliharibiwa vibaya na zaidi ya nyumba 10 za kulala wageni ndani ya kambi zimefurika baada ya Mto Talek ulio karibu kuvunja kingo, huku kukiwa na hofu kwamba huenda kuna baadhi ya wanyama walisombwa na mafuriko hayo.

"Maji yamepungua lakini baadhi ya nyumba za kulala wageni na kambi bado ziko chini ya maji," alisema Lotiatia.

Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya lilisema haijulikani ni watu wangapi wamenaswa katika hifadhi hiyo, lakini takribani 36 wameokolewa hadi sasa kwa ndege na wengine 25 na timu ya uokoaji ya mashua.

"Katika baadhi ya kambi, mahema yamesombwa na maji, na daraja la Mara, linalounganisha Mara Trianglena Greater Mara, limesombwa na maji," shirika hilo la misaada lilibainisha.

Lotiatia awali aliwaambia wanahabari kwamba timu za uokoaji zilikuwa zikitumia helikopta mbili za dharura kuwahamisha watalii na wafanyakazi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa hali imekuwa mbaya zaidi kutokana na maji yanayotiririka kutoka Mto Mara, karibu na mpaka wa Serengeti na Tanzania, kutokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha katika eneo hilo.

"Baada ya siku kadhaa za mvua zinazoendelea kunyesha, mito yetu imejaa maji na kuathiri kambi na maeneo kadhaa katika Hifadhi ya Kitaifa ya Maasai Mara. Barabara na madaraja pia yamezamishwa na maji, na kuathiri jamii zinazoishi huko," serikali ya kaunti ya Narok ilisema kupitia taarifa.

**WAKIMBIZI 20,000 WAATHIRIKA**

Shirika la Wakimbizi Duniani, (UNHCR) nchini Kenya, lilisema zaidi ya wakimbizi 20,000 wameachwa bila makao baada ya nyumba zao kuharibiwa na mafuriko hayo kwenye kambi kubwa ya Dadaab.

Katika taarifa ya shirika hilo limesema kuwa sasa wakimbizi hao wanaishi kwenye madarasa ya shule saba mbali na sehemu iliyokumbwa na mafuriko ambako vyoo vimefurika maji na kuna hatari ya kutokea magonjwa yanayosababishwa na maji machafu.

Korad Abdiwanhab, ni mmoja ya wakimbizi waliolazimishwa kuhama walipokuwa wanaishi kutokana na mafuriko.

"Maji yaliingia kwenye nyumba kutoka pande zote Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Mara tu nilipoona maji yameingia niliamka ghafla na kumwamsha mtoto wangu mlemavu na watoto wengine," alisema Abdiwanhab.

Katika eneo la Dadaab kuna kambi tatu za wakimbizi ambazo ni makao ya wakimbizi 1,240. ***Chanzo mitandao ya kimataifa***



Wakazi wa Nairobi wakijaribu kukusanya mali zao zilizosombwa na maji ya mafuriko nchini Kenya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Wakazi wa Kenya wakiendelea kuokoa mali zao baada ya makazi yao kujaa maji ya mafuriko.

> **Maji yaliingia kwenye nyumba kutoka pande zote Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Mara tu nilipoona maji yameingia niliamka ghafla na kumwamsha mtoto wangu mlemavu na watoto wengine**

# GUEDE AMKOSHA GAMONDI

**Na Faustine Feliciane**

HUKU akishuhudia timu yake ikipata ushindi mwingine ugenini, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anafurahishwa na aina ya wachezaji alionao kwa namna wanavyojituma na kufanya mambo kuwa mazuri kwa upande wao huku akielezea namna anavyokunwa na mwendelezo wa makali ya straika, Joseph Guede.

Yanga ikiwa ugenini mkoani Kigoma iliibuka na ushindi wa bao 1-0 juzi dhidi ya wenyeji wao Mashujaa FC na kuendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 65 baada ya kucheza michezo 25 mpaka sasa.

**Akizungumza jana, Gamondi alisema anafurahishwa na ubora wanaouonyesha wachezaji wake na kuifanya timu kuendelea kupata matokeo mazuri kwenye michezo ya Ligi Kuu inayoelekea ukingoni.**

"Tumekuwa na kiwango kizuri, tumetoka kwenye mashindano ya kimataifa, lakini bado wachezaji wangu wananipa kile ninachokitarajia, kila mmoja anatekeleza vizuri majukumu yake uwanjani, ni jambo ninalojivunia sana," alisema Gamondi.

Aidha, alisema licha ya kucheza mechi katika muda mfupi mfupi, bado wamekuwa na mwendelezo wa matokeo mazuri kutokana na uwajibakaji wa wachezaji wake kwa kila anayepata nafasi ya kucheza.

Kocha huyo alisema licha ya kila mchezaji kuonyesha uwezo mkubwa, lakini anafurahishwa zaidi na mshambuliaji wake, Guede, ambaye amekuwa na mwendelezo mzuri wa kufunga kila anapopata nafasi ya kucheza.

"Ni mchezaji mzuri na navutiwa na kila anachokifanya, kila anapopata nafasi anakupa kitu unachokitaka, amekuwa na mwendelezo mzuri sana, anapambana na kutumia nafasi vizuri kila anapopata," alisema Gamondi.

Matokeo ya juzi yanaifanya Yanga kusaka ushindi kwenye michezo miwili na angalau sare moja kuweza kutetea kwa mara ya tatu ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC.

Pointi nane pekee zinaweza kuwatangazia ubingwa kwa kuwa watakuwa wamefikisha alama 73 ambazo haziwezi kufikiwa na Azam au Simba wanaoshika nafasi ya pili na ya tatu hata wakimaliza michezo yao yote kwa ushindi.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah (katikati), akiongoza wachezaji wa klabu za Jogging wilayani hapo kwenye mazoezi ya viungo yaliyofanyika katika Uwanja wa Jitegemee, Muheza juzi na kisha kuzunguka mitaa mbalimbali kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ili kujikinga na magonjwa yasiyo ambukiza. Alisema mazoezi hayo yatakuwa endelevu kila Alhamisi ya mwisho ya mwezi. Kulia ni Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki. Miongoni mwa Klabu za Jogging zilizoshiriki mazoezi hayo ni Muheza Jogging Sports, Fighter Jogging na Muheza High School. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Baadhi ya wachezaji wa Simba Queens

# *Simba Queens bado nne kutwaa ubingwa 2023/24*

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Simba Queens, kinahitaji pointi nne tu katika mechi nne zilizobakia za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ili kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Simba Queens ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 40 na katika msimamo wanafuatiwa na mabingwa watetezi, JKT Queens, zote za Dar es Salaam, yenye alama 31. Endapo JKT Queens inayonolewa na mshambuliaji wa zamani wa Twiga Stars, Esther Chabruma, itashinda mechi zake zote nne zilizosalia msimu huu itafikisha pointi 43.

JKT Queens ilijiondoa katika mbio za kuwania taji hilo baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Simba Queens katika mechi iliyochezwa Aprili 29, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10, inashikiliwa na Ceasiaa Queens ya Iringa yenye pointi 26, na kama itashinda michezo yake minne iliyobakia itafikisha alama 38.

Bunda Queens ya Mara, Baobab Queens (Dodoma), Alliance Girls (Mwanza) na Geita Gold Queens ya Geita inayoburuza mkia katika msimamo ziko kwenye hatari ya kushuka daraja.

Bingwa wa Ligi ya Wanawake Tanzania ataiwakilisha Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika baadaye mwaka huu na timu itakayobeba taji hilo ndiyo itakayoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## JKU yakaa kileleni ikikiri ligi ya Zanzibar moto

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu ya JKU, Salum Ali Haji, amesema mchuano wa mbio za ubingwa Ligi Kuu Zanzibar unazidi kushika kasi kadri michezo ya ligi hiyo inavyoelekea ukingoni.

JKU SC imefanikiwa kurudi tena kileleni baada ya kuifunga Mlandege FC bao 1-0 katika mchezo wa mzunguko wa 22 wa ligi hiyo, hivyo kufikisha alama 47 huku wapinzani wao wa karibu KMKM SC wakiwa na pointi 45 wakati nafasi ya tatu ikishikiliwa na Zimamoto SC kwa alama zao 43.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema katika hatua hii iliyobaki ambayo kila timu imebakisha michezo nane kumaliza ligi hiyo, hakuna mchezo rahisi kila unaposhuka uwanjani.

"Michezo yote hivi sasa ni migumu mno, kila timu imerudi kivingine kabisa uwanjani, kila mchezo hauna tofauti na fainali ambayo matokeo ya mwisho ya ushindi ndio yanahitajika," alisema.

Aidha, alisema njia pekee ya kuweza kupambana na hali hiyo ni kuendelea kukiandaa kikosi chake vizuri kwa kila mchezo ili kuhakikisha hakipotezi malengo.

## Mtibwa kupigania nafasi yao Ligi Kuu Bara

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya matokeo mabaya wanayoyapata kwenye michezo ya Ligi Kuu, uongozi na benchi la ufundi la Klabu ya Mtibwa Sugar, wamesema watapambana katika michezo iliyobaki kuhakikisha timu inabaki kwenye ligi msimu ujao.

Mtibwa inaburuza mkia ikiwa na pointi 17 pekee baada ya kucheza mechi 25 na katika michezo miwili ya mwisho iliyocheza jijini Dar es Salaam imekumbana na vipigo kutoka kwa JKT Tanzania na Simba.

Kocha wa timu hiyo, Zuberi Katwila, alikiri kuwa kwenye wakati mgumu, lakini bado hawajakata tamaa kuipambania timu kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Alisema anafahamu matokeo wanayoyapata si mazuri na kama benchi la ufundi wanajitahidi kuweka mambo sawa kwenye michezo iliyobaki ili wabaki Ligi Kuu.

"Hatujakata tamaa, matokeo si mazuri kweli tunayoyapata, wachezaji wanafahamu sehemu tulipo sasa si nzuri, kwa pamoja tutapambana katika mechi zilizobaki kuhakikisha tunatoka hapa tulipo sasa," alisema Katwila.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMUUZA JESUS

ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa za kumuuza mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### PARTEY ATAKIWA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, na Gabriel Jsus wanasemekana kuwa kwenye rada za klabu kadhaa nchini Saudi Arabia. ***(Express)***

### WILSON SASA HAKIELEWEKI

MUSTAKABALI wa mshambuliaji wa Newcastle United, Callum Wilson, bado haujulikani huku Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 32, akihusishwa na uwezekano wa kuondoka pale St James' Park. ***(Mirror)***

### TUCHEL NA MAN UNITED

KOCHA anayeondoka Bayern Munich, Thomas Tuchel, ndiye anayeongoza kuwania nafasi ya kocha ajaye wa Manchester United huku klabu hiyo ya Ligi Kuu England ikilenga kuiziba nafasi ya Erik ten Hag. ***(Football Insider)***

### SANCHO KUBAKI DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inataka kusalia na winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo msimu ujao, kwa sababu uhamisho wa kudumu kutoka Manchester United kwa sasa hauwezekani na gharama yake ni ya juu kwa klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Sky Sport Ujerumani)***

### MAN FEDHA KIBAO

KLABU ya Manchester United inatumaini kupata pauni milioni 100 kwa kumuuza mshambuliaji Jason Sancho na Mwingereza Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa majira ya joto. ***(Give Me Sport)***

### GUIRASSY ALENGWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Stuttgart kutoka Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 28, ameonekana kulengwa na Arsenal wakati huu Mikel Arteta akijaribu kuimarisha safu yake ya ushambuliaji. ***(Fichajes)***

### PHILLIPS NA LEEDS

MATUMAINI ya kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips kuungana tena na Leeds United msimu huu wa majira ya joto yanategemea timu hiyo ya Elland Road kupata nafasi ya kurejea Ligi Kuu. ***(Football Insider)***

### HERMOSA AWINDWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inakaribia kumsajili beki wa Atletico Madrid, Mario Hermoso mwenye umri wa miaka 28. ***(AS)***

### DAVID ATAKIWA MILAN

KLABU ya AC Milan ipo tayari kufikiria kumsajili mshambuliaji wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, kutoka Lille katika dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomerca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SLOT ATHIBITISHA KUTUA LIVER KUMRITHI KLOPP

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Feyenoord, Arne Slot, amefichua kuwa anatarajia tangazo la hatima yake litatolewa hivi karibuni anapojiandaa kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp katika Klabu ya Liverpool.

**'Wekundu' hao walikubaliana na Slot mwezi uliopita na wakafikia makubaliano yenye thamani ya euro milioni 15 na Feyenoord ili kumwajiri bosi huyo wa Uholanzi na wasaidizi wake wachache.**

Liverpool walirejea katika njia ya ushindi Jumapili kwa kushinda mabao 4-2 dhidi ya Tottenham Hotspur, na Slot alikiri kuwa alitazama mwanzo wa mechi kabla ya kuwaongoza Feyenoord dhidi ya PEC Zwolle.

> Wakati mwingine maishani fursa zinakuja na lazima usikilize, nimeamua...

"Niliona dakika chache za mchezo, lakini ilibidi tuje uwanjani," alifichua.

"Bao la kwanza tu, bao kubwa. Ulikuwa ushindi mzuri kutoka kwa Liverpool. Ikiwa uthibitisho rasmi upo, na niende huko, nitatazama michezo mingi kutoka kwao.

"Wakati mwingine maishani fursa zinakuja na lazima usikilize, nimeamua mwenyewe, siku na wiki zijazo utaona tangazo.

"Mwaka jana nilifanya chaguo la kubaki na sasa labda nilifanya chaguo lingine."

Aliongeza: "Sina wasiwasi hata kidogo kama itaendelea - swali ni lini itawasilishwa."

Baada ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya PEC Zwolle, Slot alionekana akiwapungia mkono mashabiki waliokuwa kwenye jukwaa huku uso wake ukioneshwa kwenye skrini kuzunguka uwanja, na bosi huyo wa Uholanzi alikiri ilionekana kama kwaheri.

"Nadhani nakubaliana na hilo, kwamba ilionekana hivyo," alisema.

"Kwa sababu ya uvumi wote kwenye vyombo vya habari nadhani wanatarajia niondoke. Ndio, hilo ni jambo ambalo tunaweza kusema."

HABARI MICHEZO

# TEN HAG AMJIA JUU MOURINHO



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amejibu maoni yaliyotolewa na Jose Mourinho baada ya kocha huyo Mreno kusema kuwa hakuwahi kuwa na "uungwaji mkono" kama Mholanzi huyo pale Manchester United.

Mourinho alipendekeza kuwa Ten Hag amepewa uungwaji mkono zaidi katika soko la uhamisho kuliko ilivyokuwa wakati wa miaka yake miwili na nusu akiwa Old Trafford.

Hata hivyo, Ten Hag amejibu kwa kudai kuwa Mourinho ndiye kocha pekee katika zama za baada ya Sir Alex Ferguson "kupata wachezaji anaowataka."

"Mbali na Mourinho, kocha mwingine hakupata wachezaji aliotaka, na hicho ndicho unachohitaji," alisema Ten Hag katika mahojiano na ESPN Brasil.

"Nina imani tutafikia malengo yetu, lakini ni mashindano magumu, si mbio za farasi wawili tena.

"Kuna saba, nane (timu kwenye Ligi Kuu) ambazo zote zinakwenda kwa ajili ya ubingwa, ambazo zote zina vikosi vizuri sana. Hivyo kama unataka kutwaa ubingwa, lazima utengeneze kikosi hicho."

Ten Hag anakabiliwa na mustakabali usio na uhakika ndani ya United baada ya kuwa na msimu wa pili usioridhisha.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake, lakini hajapewa hakikisho rasmi na mmiliki mwenza mpya Sir Jim Ratcliffe kama ataendelea kuwa kocha zaidi ya msimu wa majira ya joto.

Kocha huyo wa zamani wa Ajax alijaribu bila mafanikio kuwasajili wachezaji kama Frenkie de Jong na Harry Kane, lakini akasema uamuzi wa klabu hiyo kuleta wachezaji wachanga kama Rasmus Højlund unamaanisha kwamba anapaswa kupewa "uvumilivu" ili kurekebisha mambo.

"Unahitaji wachezaji bora," alisema Ten Hag.

"La sivyo, uko kwenye mchakato na lazima uwe na subira. Hapo ndipo tulipo."

## Pogba ageukia kucheza muvi

**PARIS,** Ufaransa

MSHINDI wa Kombe la Dunia, Paul Pogba, ataigiza katika filamu ya Ufaransa itakayotolewa Aprili 2025 baada ya kurekodi matukio ya video mjini Paris wiki hii, vyanzo vimeiambia ESPN.

Pogba anatumikia kifungo cha miaka minne kwa ukiukaji wa matumizi ya dawa za kusisimua misuli ambayo ilitolewa Februari mwaka huu.


Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa, alisema wakati huo kuwa hajawahi kuchukua kwa makusudi dawa zilizopigwa marufuku na alipanga kukata rufani dhidi ya uamuzi huo.

Filamu hiyo inaitwa 4 Zeros, na ni mwendelezo wa 3 Zeros iliyotolewa mwaka 2002.

Kwa mujibu wa Jarida la Ufaransa la Le Parisien, ambalo liliripoti kwa mara ya kwanza kuhusu nafasi ya Pogba katika filamu hiyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, atacheza kama kocha wa timu ya vijana.

Rufani ya Pogba kuhusu shtaka hilo la matumizi ya dawa za kusisimua misuli litasikilizwa na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS), na iwapo rufaa yake itafanikiwa, adhabu yake inaweza kupunguzwa.




## *Roque hana furaha Barca - Wakala*

**BARCELONA,** Hispania

WAKALA wa Vitor Roque, Andre Cury, amesema haelewi ni kwa nini mshambuliaji huyo wa Brazil amekuwa akitumiwa kwa kiasi kidogo na Barcelona na kupendekeza kwamba anaweza kuondoka katika majira ya joto ikiwa hali hiyo haitatatuliwa.

Roque mwenye umri wa miaka 19, alijiunga na Barca kwa kitita cha Euro milioni 31 kutoka Athletico Paranaense Januari na tangu wakati huo amefunga mabao mawili katika mechi 13, nyingi akitokea benchi.

Kinda huyo amekuwa mchezaji wa akiba ambaye hakutumika katika mechi nne za mwisho za Barca, tatu kati yake walipoteza, na sasa wakala wake, Cury amesema Roque hana furaha.

"Vitor Roque anapaswa kuwa na dakika zaidi na hakuna anayeelewa kwa nini hapati," alisema Cury akiiambia RACI.

"(Kocha wa Barca), Xavi Hernandez hajawahi kuzungumza na mchezaji na sielewi hali hiyo. Sio nzuri kwa mtu yeyote.

"Mtoto anapaswa kufanya kazi kwa bidii na kusubiri nafasi yake, lakini tayari kumekuwa na michezo mingi ambayo angeweza kupewa dakika hizi na jukumu kubwa zaidi.

"Katika dakika 300 alizocheza, amefunga mabao mawili, ambayo inawezekana ni kiwango bora zaidi katika timu. Xavi ametoa nafasi kwa Fermin Lopez, Pau Cubarsi na Lamine Yamal, lakini si kwa Vitor Roque."

Cury pia alisisitiza kwamba ilimchukua Vinicius Junior muda kuwa mchezaji wa muhimu katika Klabu ya Real Madrid baada ya kujiunga nayo mwaka 2018, awali akiichezea timu ya akiba, lakini akasema waandishi wa habari huko Barcelona hawampi Roque subira kama hiyo.

"Barcelona, kuna vyombo vingi vya habari ambavyo vinazungumza machafu na kusema mambo ambayo si ya kweli," alisema Cury.

"Haisaidii. Angalia kilichotokea kwa Vinicius huko Madrid. Alichukua miaka miwili na nusu kucheza mara kwa mara. Hapa Barcelona ni tofauti."

# HABARI MICHEZO

## Simba, Ibenge kimeeleweka

INATOKA UKURASA 24

Alisema watapitia ripoti ya benchi la ufundi lililopo chini ya Juma Mgunda pamoja na Kamati ya ufundi na kuweka wazi kuwa baada ya msimu huu kumalizika watapitia ili wajue ni sehemu gani za kupaboresha.

"Ninaomba Wanasimba wasiwe na wasiwasi msimu ujao tutafanya mabadiliko ambayo yatamwacha wazi kila mtu, tumedhamiria makubwa tunataka turudishe heshima yetu ya mwanzo," alisema.

## Yanga yanasa beki 3 wa DRC

INATOKA UKURASA 24

timu nchini Afrika Kusini.

Habari zinasema kumekuwa na mvutano kati ya Augustine Okrah na Kennedy Musonda nani anatakiwa kuachwa kwa ajili ya kupisha usajili wa mchezaji mwingine ili kukiimarisha kikosi hicho.

Wakati huo huo, kocha Gamondi ametamba kuwa timu yake inahitaji pointi tatu katika kila mechi ili kutwaa ubingwa, hivyo hatoangalia ukubwa au udogo wa mchezo.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo na Mashujaa FC, uliochezwa Uwanja wa Lake Tanganyika juzi na Yanga kushinda bao 1-0, Gamondi alikiri kuwa mechi ilikuwa ngumu mno, lakini kwa sababu kila mmoja anajua kuwa wanahitaji ubingwa, ushindi ukapatikana.

"Mashujaa FC ni timu nzuri, imepambana sana, mechi ilikuwa ngumu kwetu na nimempongeza kocha wao, ila walikuwa hawajui kuwa wanacheza na timu inayohitaji matokeo zaidi kwa sasa kuliko kipindi kingine chochote.

"Kipindi cha kwanza tulikuwa na mchezo mzuri, tulimiliki mpira, tulitengeneza nafasi, tukafunga bao moja ambalo ni muhimu.

Kipindi cha pili wapinzani wetu walikuja juu, bila shaka walitaka kurudisha bao, walihitaji pointi, walipiga mipira mirefu na krosi nyingi, nadhabni walikuwa vizuri kuliko sisi, kilichoamua matokeo ni uzoefu na dhamira, ninashukuru kupata pointi tatu ugenini, hasa kwa uwanja kama huu," alisema Muargentina huyo.

Naye kocha Mohamed Abdallah 'Bares', wa Mashujaa FC aliwasifu vijana wake, akisema ni kosa moja tu ndilo lililowahukumu.

"Tumecheza vizuri, kipindi cha kwanza tulikuwa na 'plani' yetu, tulijaribu sana kuzuia, kwa sababu unajua Yanga ni timu ambayo mchezaji mmoja mmoja anaweza kuamua matokeo, kwa hiyo tuliingia na tahadhari, tukafanya kosa moja wakatuhukumu," alisema.

# MWANA FA: TUKUTANE BETIKA MBEYA TULIA MARATHON 2024

**Mwanadishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, amefichua namna alivyojipanga kukimbia kwenye mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathon msimu huu, akiwataka wadau wa riadha nchini wakutane Mbeya zinapofanyika mbio hizo.

**Mwana FA amesema yuko fiti kukimbia na kumaliza mbio ndefu kwenye msimu wa saba wa Betika Mbeya Tulia Marathon Ijumaa na Jumamosi hii pale kwenye Uwanja wa Sokoine.**

Akizungumza katika mbio za amshaamsha ambazo ni maalum kwa ajili ya maandalizi kuelekea Mbeya, Mwana FA aliyewaongoza mamia ya wanariadha wa jijini Dar es Salaam kwenye amshaamsha hiyo alisema, morali ambayo wanariadha hao wameionyesha hakuna shaka Mbeya ushindani utakuwa mkali.

Mbio za Betika Mbeya Tulia Marathon zinazolenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu zitaongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Zaidi ya wakimbiaji 5000 watakimbia kusaka mabingwa wa marathon (kilomita 42), nusu marathon (kilomita 21) kilomita 10 na kilomita tano Jumamosi wiki hii, ikiwa ni siku moja baada ya mbio za uwanjani za mita 100, 200, 400, 800 na 1500.

Japo hakusema atakimbia mbio gani, Naibu Waziri huyo alisema atakimbia mbio ndefu na hana shaka atafanya vizuri, kauli kama iliyowahi kutolewa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson katika amshaamsha kama hiyo iliyofanyika jijini Dodoma hivi karibuni, akibainisha yuko fiti kwa marathon na atashinda medali.

Katika amsha amsha hiyo iliyoanzia kwenye ukumbi wa mikutano wa Julius Nyerere, Posta hadi kwenye fukwe za Coco, Mwana FA alibainisha alivyofiti kukimbia na kumaliza mbio ndefu bila kueleza ni za kilomita 10, 21 au 42.

"Tukutane Mbeya, niko fiti, kama Dar es Salaam nimekimbia na kumaliza umbali mrefu, kule Mbeya mjipange," alisema Naibu Waziri huyo akishangiliwa kwa nguvu huku baadhi ya wanariadha wa Dar es Salaam wakiahidi kurudi na ubingwa.

Baadhi ya wanariadha wa Dar es Salaam wamepata udhamini wa Betika kwenda kuchuana jijini Mbeya wakilipiwa usafiri na gharama nyingine, ikiwa ni sehemu ya kampuni hiyo ya michezo ya kubashiri matokeo ambao ndio wadhamini wakuu wa kuzinogesha mbio hizo msimu huu.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema amshaamsha hiyo kesho Jumatano itafanyika jijini Mbeya, ikiwa ni baada ya mikoa ya Mtwara, Rukwa, Iringa, Morogoro na Dodoma kufanya tukio kama hilo kama sehemu ya maandalizi ya kushiriki mbio za msimu huu.

Alisema, Betika itawagharamia wanariadha 460 kushiriki mbio hizo msimu huu, kuongeza hamasa na kutoa fursa kwa wale wenye vipaji kuonekana.




Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, akiwakabidhi bendera ya mabingwa baadhi ya wanariadha wa Dar es Salaam jana, watakaokimbia mbio za Betika Mbeya Tulia Marathon Ijumaa na Jumamosi wiki hii jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Nyota Taifa Stars waipa Yanga FA Cup*

**Na Somoe Ng'itu**

NYOTA wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Adolph Rishard na Dua Said, wameipa nafasi kubwa Yanga kutetea ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA ambalo kwa sasa limeingia hatua ya nusu fainali.

Yanga itacheza hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu FC, mechi itakayochezwa Mei 19, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Nusu fainali nyingine ya michuano hiyo inayodhaminiwa na Benki ya CRDB itawakutanisha Azam FC na Coastal Union, mchezo utaopigwa Mei 18, mwaka huu, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza jijini jana, Rishard alisema Yanga kwa sasa iko 'moto' na haoni kama kuna timu inaweza kuizuia isibebe ubingwa wa michuano hiyo.

Alisema wachezaji wa Yanga wamekuwa na morali kubwa na kila anayepata nafasi ya kucheza anapambana kuonyesha kiwango bora ili kufikia malengo ya timu yao.

"Kiukweli Yanga kwa sasa wako moto, wako 'on fire', mimi kwa maoni yangu nawaona wakienda kubeba ubingwa wa michuano hii", alisema nyota huyo wa zamani wa Pan African.


Naye mshambuliaji wa zamani wa Simba, Saidi alisema Yanga iko katika ubora mkubwa na kama haitatokea vinginevyo, ubingwa wa michuano hiyo utatua klabuni kwao.

Mshambuliaji huyo alisema matokeo mazuri wanayopata Yanga katika Ligi Kuu Tanzania Bara yamekuwa ni chachu ya kufanya vizuri pia katika michuano hiyo.

"Kwa macho yangu nawaona Yanga wakienda kushinda tena taji hili, labda itokee vingine kwa sababu katika mpira lolote linaweza kutokea," aliongeza mshambuliaji huyo.

Fainali za mashindano hayo ambazo bingwa wake ataiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya Kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao, itafanyika Babati mkoani, Manyara.

Michezo
Jumanne Mei 7 2024
Nipashe



Slot athibitisha kutua Liver UKURASA 21

HUWEZI...



Winga wa Liverpool, Luis Diaz, akijaribu kufunga lakini Kipa wa Tottenham Hotspur, Guglielmo Vicario, akawa makini kuokoa, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Anfield juzi na Liver kushinda mabao 4-2. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yanasa beki tatu wa DR Congo

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akitamba kuwa dozi zitaendelea kama kawaida kwenye mechi za Ligi Kuu, licha ya kukutana na upinzani mkali kwa baadhi ya timu, klabu hiyo ipo katika hatua za mwisho kumsainisha beki Chadrack Boka kutoka Klabu ya Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Taarifa zilizopatikana jana zinaeleza kuwa Yanga ipo karibuni kupata saini ya mchezaji huyo anayecheza nafasi ya beki wa kushoto, ili kuchukua nafasi ya Joyce Lomalisa ambaye huenda akaondoka mwishoni mwa msimu, lakini ikiwa ni pendekezo la kocha Gamondi.

Mtoa taarifa huyo amesema Rais wa Yanga, Hersi Said, yupo nchini humo kwa ajili ya kusaka baadhi ya wachezaji wa kuimarisha kikosi kuelekea msimu ujao wa mashindano.

Imeelezwa kuwa Hersi pia amekutana na Rais wa Klabu ya TP Mazembe, Moise Katumbi kwa lengo la kuzungumza na kujadilia mambo mbalimbali ikiwamo uendeshaji wa timu, lakini na suala zima la usajili wa wachezaji.

"Siyo huyo tu, kocha ametoa mapendekezo ya wachezaji kadhaa na suala la straika ndiyo limezingatiwa zaidi maana tangu alipoondoka Mayele (Fiston), hajapatikana mtu sahihi, waliokuja bado hawajaweza kukidhi mahitaji ya safu hiyo, pia tunaendelea kuimarisha safu ya ulinzi," alisema mtoa habari huyo.

Yanga ipo katika mipango ya kuachana na baadhi ya nyota wake, ambapo mbali na Lomalisa, yupo Mahlatse Makudubela maarufu kama 'Skudu' na Bakari Mwamnyeto ambaye hataongezewa mkataba, taarifa zikisema wakala wake amemtafutia

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Ibenge kimeeleweka

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

## Aomba rasmi kuondoka Al Hilal, pia wanasa wakata umeme wawili kutoka Guinea huku ikitamba...

KLABU ya Simba iko katika nafasi nzuri ya kumtwaa kocha Florent Ibenge, baada ya mwenyewe kuomba kuondoka ndani ya timu ya Al Hilal ya Sudan, huku uongozi wa timu hiyo ukiendelea kupambana kumbakisha.

**Wakati hayo yakiendelea, Klabu ya Simba iko mbioni kuwasajili wachezaji wawili wa timu ya Hafia FC ya Guinea, Mohamed Damaro Camara mwenye miaka 21, na Ousmane Fernandez 'Drame', 23.**

Taarifa zilizopatikana jana kutoka vyanzo tofauti vya habari za michezo Afrika, zinaeleza kuwa kocha huyo amekaa vikao viwili na mabosi wa Al Hilal wakimweleza kuwa wana imani naye, lakini mwenyewe amesisitiza kuwa anataka kuondoka na sababu kubwa ni kutaka kuifundisha timu inayocheza Ligi Kuu na kupambania mataji.

"Kwenye majadiliano ya hatima yake, viongozi wamemweleza kocha kuwa bado wana imani na utendaji wa kazi yake na wanataka kuendelea naye, lakini ameng'ang'ania kuondoka kwa sababu timu kwa sasa haichezi ligi kutokana na machafuko yanayoendelea nchini Sudan," vilisema vyanzo hivyo.

Licha ya kwamba Al Hilal huenda ikacheza Ligi Kuu Tanzania Bara nchini, baada ya maombi yao kukubaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), lakini kocha huyo bado anaonekana hajaridhika na hilo.

Ibenge anatajwa kuwa kwenye orodha ya wanaotakiwa na Klabu ya Simba na kupewa nafasi kubwa ya kuwa kocha mkuu, baada ya kuondoka, Abdelhak Benchikha, huku kitendo cha kuomba kuondoka Al Hilal kikionekana kuwa huenda tayari ameshafikia makubaliano na klabu hiyo.

Hii si mara ya kwanza kwa klabu hiyo kumhitaji Ibenge ambaye raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ilibaki kidogo imnase mwaka 2022, lakini ilishindikana na kuangukia kwa Zoran Maki.

Pamoja na kusaka kocha, Klabu ya Simba imepiga hodi nchini Guinea, ikiwa katika harakati za kuwasainisha viungo wawili, Camara na Drame, ambao wanatajwa kuja kuchukua nafasi ya Sadio Kanoute anayedaiwa kuomba kuondoka mwishoni mwa msimu, pamoja na Fabrice Ngoma.

Usajili huo umetajwa ni kwa ajili ya kuimarisha eneo la kiungo, ambapo Camara anacheza nafasi ya kiungo mkabaji, huku Drame, akiwa na uwezo wa kucheza namba sita, na nane.



Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema kila kitu kinakwenda vizuri, lakini hivi sasa siyo wakati wa kuzungumzia kitu chochote kuhusu kocha au usajili kwani akili yao ni kusaka nafasi mbili za juu ili msimu ujao wareje kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunaleta kocha bora, na tutafanya usajili mkubwa safari hii, mashabiki wetu watulie, kwa sasa si wakati wake, kwanza tuungane, tushikane ili kupate nafasi ya kurejea tena kule tulikozoea," alisema Ahmed.

Alisema watafanya maamuzi magumu kwa lengo la kuiboresha timu yao na kuahidi kuwafurahisha mashabiki wao kutokana na usajili watakaoufanya.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >